**Wosia** aliyejichinja shingo kwa mashine ya mbao watimizwa

UKURASA 4



**Utafiti** wabaini mifugo inayocheua ni hatari kuongeza joto duniani

UKURASA 13



Ukurasa 12

Waliokatiza masomo waambiwa kila kitu kipo, wachangamkie shule

Ukurasa 14

Nishati safi jikoni kwa kila Mtanzania inawezekana, Umoja wa Ulaya wajitosa

Nipashe TESA

Jumanne Juni 20, 2023

TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

Ukurasa 13

Singapore yawa taifa pekee kunapoliwa kitoweo cha kutengenezwa maabara

TEKNOLOJIA NA PILLY KIGOME

ROSETTLE LOWHIM

Injinia aliyeshinda usaili lakini akatoswa ajira, kisa mwanamke

• Ni mgunduzi mahiri akihusika na jiko sanifu

ROSETTLE Lowhim ni mwanafunzi wa shahada ya uzamivu ya uhandisi katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam [DIT], ambaye amekuwa pambo na chachu kwa wengine kwa namna anavyojitahidi kuitumia teknolojia kubadilisha maisha yake na ya wengine.

Akiwa bado masomoni ameunda mashine kadhaa zinazotumiwa na mafundi vyuma anaposema mwaka 2021 hadi 2022 akiwa mwaka wa tatu wa shahada ya kwanza ya Uhandisi Mitambo (mechanical engineering) alibuni na kutengeneza mashine za urembo unaotokana na kukunja vyuma.

Anaitambulisha kama 'semi automatic metal scrolling and twisting machine' inayotumiwa kukunja vyuma kutengeneza urembo kwenye madirisha ya grili, milango, mageti na mapambo mbalimbali.

Mara nyingi urembo wa madirisha, vitanda, milango, meza, uzio na mapambo mengine hutengenezwa kwa kukunja na kusuka nondo au 'square pipes na flat bars na pengine hakukuwa na mashine ya kuzikunja kupata maumbo mbalimbali bali kazi hizo hufanyika kienyeji.

Rosettle anasema mbali na mashine hiyo pia amegundua na kutengeneza nyingine ya kubangua karanga [groundnut cracking machine] ambayo tayari iko sokoni.

Kadhalika anasema amebuni jiko maalum la umeme la kukaangia crips na chips linalotumia nishati kidogo lakini likifanyakazi kwa ufanisi mkubwa na kusaidia kupunguza matumizi ya mkaa na kuni yanayochangia kuharibu misitu na kuchochea mabadiliko ya tabianchi.

**ANATAJA PAGUMU**

Msomi anakumbushia kuwa licha ya juhudi na jitihada za kufanikisha maendeleo ya sayansi na teknolojia, anakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na kutoaminika kwenye ajira kwa vile ni mwanamke, hivyo kukosa kazi.

Anasema kutokana na jinsi yake mbali na kuwa na uwezo mkubwa kufanya vizuri katika kazi lakini inamuwia vigumu kuaminika kikazi jambo linalomshangaza na kumuumiza msomi huyo.

Anaendelea kuiambia Nipashe kuwa, amewahi kukosa kazi kutokana na jinsi yake (KE) katika moja ya kampuni kubwa nchini (jina tunalihifadhi) alipokwenda kufanya usaili.

Anasema aliambiwa kuwa amefaulu kwenye usaili lakini baadaye mkuu wa kampuni alipogundua ni mwanamke, akamkataa akakosa kazi hiyo, japokuwa alifanya vizuri katika usaili na kuibuka kidedea.

Rosettle anafafanua kuwa ndoto zake kubwa ni kuja kumiliki karakana ama kampuni kubwa ya kisasa nchini itakayoweza kuhudumu ndani na nje ya mipaka kwenye masuala ya teknolojia na uhandisi.

Mhandisi Rosettle Lowhim wa DIT akiwa kazini kutengeneza mashine ya kubangulia karanga. **PICHA: MWANDISHI WETU**

**KUCHOCHEA WANAWAKE**

Ubunifu na mabadiliko ya teknolojia ni chachu ya kuleta usawa wa kijinsia, ni kauli mbiu ya kitaifa inayotumiwa kuwachochea wanawake kama sio kuwatoa kimasomaso mijini na vijijini katika kujihusisha na kunufaika na teknolojia.

Lengo ni ili usawa unapatikane kupitia nyanja hiyo, na kuwaamsha wanawake wengi ambao wamebaki nyuma na kukosekana usawa kiteknoloji na hata kijinsia.

Mtandao wa Jinsia Tanzania [TGNP] na Chuo cha DIT, wanaingia ubia kusaidia kufanikisha kazi za ubunifu za kiteknolojia na kutatua changamoto za kijinsia kama sehemu ya kuwapa fursa na hamasa wasichana wanafunzi kufanya vizuri katika eneo hilo 76la sayansi na teknolojia.

Taasisi hizi zimetengeneza kanzi data inayoitwa Tanzania Women Connect Portal inayohifadhi kazi za wanawake katika nyanja mbalimbali itakayowezesha kupata na kunufaika na fursa mbalimbali kwenye harakati za kuleta usawa wa kijinsia nchini.

Mwenyekiti wa Bodi TGNP, Gemma Akilimali, anaambia Nipashe kuwa kuwawezesha wanawake na makundi mengine katika teknolojia kuna matokeo chanya hasa katika ubunifu ili kupata suluhisho kwa shida za kijamii na uvumbuzi mwingine unaowasaidia wanawake na watoto wa kike kupata mahitaji ili kuchochea ufikiwaji wa usawa wa kijinsia.

UKURASA 11

# Nipashe

Jumanne Juni 20, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • Na. 0581347

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



SAKATA LA BANDARI

# Wadau waja na hoja zao

UKURASA 2



Huko nyuma tulikubaliana sera serikali iondoke huko kwenye uendeshaji wa biashara. Nimesikiliza mijadala ya uendeshaji wa Bandari. Sina tatizo na mjadala, wala watu wanaokosoa.

**ROSTAM AZIZ**



Haya mambo ya uwekezaji yalianza zamani, tangu tulipoamua kufikiria kufanya mabadiliko ya kisiasa ya kujitawala bila kutumia silaha. Watanzania wakasema lazima nchi iwe huru. Wakatafuta viongozi wao bila ubaguzi wa dini na ukabila wowote.

**PADRI CHARLES KITIMA**



Mjadala wa Bandari ni muhimu. Vietnam mwaka 1984 ilikuwa kama Tanzania, tulikuwa tunapishana kidogo. GDP ilikuwa dola bilioni 18. Tanzania ilikuwa dola bilioni 13.8. Mwaka 1986 wenzetu waliamua kufanya mageuzi ya kiuchumi.

**ANGELINA NGALULA**



Mabadiliko ya kisiasa na kiuchumi ndio mwendo mzuri. Yanapaswa kwenda mbele na juu zaidi. siyo mabadiliko ya kusuasua. Kesho yako inapaswa kuwa bora zaidi kuliko jana yako.

**JENERALI ULIMWENGU**



Endapo mkataba utakuwa na tija, basi majadiliano ya kuongezwa eneo la uendeshaji yatafanyika. Upinzani wanajenga hoja kuwa CCM inauza Bandari. Hakuna suala la mauzo siyo tu Bandari bali sehemu ya ndani ya nchi haiwezi kuuzwa.

**PROF. KILILA MKUMBO**

## Chongolo kupeleka kwa waziri kilio cha waziri

UKURASA 3

# 150 wanaosomea udaktari Sudan wahamishiwa kumalizia Muhimbili

UKURASA 3

MICHEZO MIQUISSONE AITOA JASHO SIMBA SC UK.24 KATUNI UK.6

# Asasi 200 zapinga muswada mabadiliko sheria ya rushwa



Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, akizungumza na waandishi wa habari nyumba kwake Tegeta jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: CARLOS BANDA**

**Na Beatrice Shayo**

MTANDAO wa Kupinga Rushwa ya Ngono Tanzania umesema haukubaliani na kifungu kidogo kilichokusudiwa kuongezwa katika kifungu cha 25(2) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Mtandao huo, Prof. Ruth Meena, alibainisha hayo wakati akisoma tamko lao kwa waandishi wa habari, alisisitiza wanapinga vikali nyongeza ya kifungu hicho na kutaka kiondolewe.

Alisema mtandao huo unajumuisha asasi 200 ambazo zimekuwa zinaendesha kampeni kubwa na kuhamasisha wananchi kuhusu sheria hiyo.

"Wanamtandao wanaopinga rushwa ya ngono nchini, kwa sauti moja tunapinga nyongeza ya kifungu hiki kinachoashiria kulinda mwenye mamlaka, kutia hatiani mwathirika na kuwanyamazisha wasiweze kuwataja wahusika," alisema Meena.

Alidai kifungu kidogo kilichokupendekezwa kuongezwa katika kifungu cha 25, kitasababisha kuwapo sheria itakayoendeleza utumiaji mbaya wa mamlaka na itanyamazisha sauti za waathirika katika uwajibikaji zaidi kwa wale wote wenye dhamana ya uongozi.

Alisema wanamtandao wanaopinga rushwa ya ngono wanaona pendekezo hilo linaashiria kumlinda mwenye mamlaka na kumtia hatiani mwathirika.

"Kifungu hiki kinampokonya mwathirika ile haki aliyokuwa amepewa katika kifungu cha 25 pamoja na haya, athari kubwa ya kifungu hiki cha nyongeza ni kusababisha kunyamazisha sauti za waathirika, ambao kwa uhakika wataogopa kutoa ushahidi kwa kuogopa kuadhibiwa," alisema.

Pia alisema mchakato unaoendelea wa maandalizi ya kurekebisha Sheria ya Kuzuia na Kupinga Rushwa usitishwe na waziri mwenye dhamana asitishe marekebisho yanayopendekezwa.

Alidai maoni ya wadau wengi hayakuzingatiwa katika mchakato huo, hali iliyosababisha kutoa tamko hilo.

Alisema kuwa katika mchakato wa marekebisho ya sheria hiyo, kifungu cha 25 cha mwanzo kibaki kilivyo na kifungu kidogo cha pili kiondolewe.

Pia walitoa wito kwa Bunge lisikubali kuridhia mapendekezo hayo kama yatawasilishwa bungeni.

"Vilevile, tunamshauri Rais Samia Suluhu Hassan, mtetezi wa haki za wanawake na watoto, asibariki sheria yenye kubeba mabadiliko tunayoyapinga endapo itamfikia mezani kwake bila madai yetu kuzingatiwa.

"Tunaona kama ni mtego kwake, sheria ilipitishwa wakati wa awamu ya nne, ikatekelezwa kwa vishindo wakati wa awamu ya tano na sasa hivi wakati wa utawala wake kama Rais mwanamke kuna mapendekezo ya mabadiliko ya kuendeleza kuwakandamiza wanawake na watoto ambao ndio waathirika wakuu kwenye suala hili la rushwa ya ngono," alisema.

# Wadau waja na hoja zao sakata la Bandari

**Na Waandishi Wetu**

UWAZI, ukweli, kushirikisha kampuni za wazawa na kusikiliza maoni ya wananchi katika uwekezaji wa Bandari ya Dar es Salaam vimetawala mjadala wa kitaifa uliowakutanisha wafanyabiashara, wanasiasa na viongozi wa dini.

Mjadala huo ulioandaliwa na Media Brains jijini Dar es Salaam jana, ulijikita katika mada ya kulinda na kutetea umoja wa kitaifa wakati wa mageuzi ya kisiasa na kiuchumi, wadau hao wakijikita zaidi kujadili mkataba wa ushirikiano kati ya serikali nchini na Dubai (IGA), kuhusu uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam.

Aliyefungua mjadala huo ni mfanyabiashara Rostam Aziz, aliyewataka Watanzania kuwa na mijadala inayozingatia misingi ya umoja wa kitaifa iliyowekwa na waasisi wa nchi.

Rostam, mfanyabiashara mkubwa nchini, alisema mjadala wa uendeshaji wa bandari umewagawa wananchi kwa kuwa ulibebwa na hisia, siasa na kibaguzi, jambo alilosema ni hatari kwa ustawi wa nchi.

"Sina tatizo na watu wanaokosoa vitu, kilichonitatanisha, kunisononesha na kunitisha ni sura ya mjadala wenyewe kuwa wa kisiasa na ushabiki. Huko nyuma tulikubaliana kuwa sera ni serikali isifanye biashara... Tulikuwa na haja ya kubadilisha sera, kuruhusu wawekezaji pamoja na kuingia kwenye mfumo wa vyama vingi.

"Hivi karibuni nimesikia mjadala wa uendeshaji wa bandari, sina tatizo na watu wanaokosoa. Kilichonisikitisha na kunitisha ni mjadala wa kiuchumi umegeuzwa na kuwa wa kisiasa," alisema.

Rostam alishauri kuwa ni vyema katika masuala ya kitaifa, watu wakajadiliana kwa hoja, ili kudumisha umoja wa kitaifa uliopo.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), Angelina Ngalula, alisema uwekezaji wa bandari ni muhimu katika kukuza uchumi, akiitolea mfano Vietnam iliyofanikiwa kukuza uchumi wake mara tano zaidi ya Tanzania kupitia kukaribisha wawekezaji wa nje.

"Hii nchi mwaka 1984 ilikuwa kama Tanzania, tulikuwa tunapishana kidogo. GDP ilikuwa dola bilioni 18. Tanzania ilikuwa dola bilioni 13.8. Mwaka 1986, wenzetu waliamua kufanya mageuzi ya kiuchumi. Mageuzi yakawa na msukumo wa mambo matatu - uwekezaji kufungua nchi, kuhakikisha wanapanua na kusukuma biashara ya kimataifa," alisema.

Kiongozi huyo wa TPSF aliitetea sekta binafsi, akisema haikwepeki katika kukuza uchumi wa nchi kwa kuwa inalipa kodi zinazoelekezwa kutoa huduma muhimu za kijamii kama afya, elimu na miundombinu.

Ngalula ambaye ni mfanyabiashara wa usafirishaji, alisema bandari ni muhimu katika kuunda mfumo kamili wa mnyororo mzima wa usafirishaji, kuanzia mzigo unakotoka hadi kwa mteja wa mwisho.

Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, ambaye kitaaluma ni mchumi, alishauri badala ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) kuingia mkataba na kampuni ya DP World, iundwe kampuni binafsi itakayoingia mkataba huo kwa niaba ya serikali.

Alisema kuundwa kwa kampuni mpya kutawawezesha Watanzania kumiliki na kuiendesha Bandari ya Dar es Salaam.

Mwandishi wa Habari mkongwe, Jenerali Ulimwengu, ambaye kitaaluma ni mwanasheria, alikosoa namna usiri katika mikataba mikubwa kitaifa unavyoibua maswali mengi kutoka kwa wananchi, akisisitiza "...ni haki ya wananchi kuhoji na ni wajibu wa serikali kujibu".

Mwanasheria ambaye ni Katibu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Padri Dk. Charles Kitima, alisema licha ya kuwapo nia nzuri ya kiserikali, bado sauti za wachache zisipuuzwe, akitaka wazawa wapewe kipaumbele katika mkataba huo wa Bandari.

"Tumeambiwa kwamba tumewekeza zaidi ya Sh. trilioni moja kwenye bandari yetu. Kwanini tusianze kuiendesha kuanzia hapo badala ya kuita wawekezaji kutoka nje?" alihoji.

Alisema hakuna namna nchi inaweza kukwepa mwekezaji, lakini jambo la msingi ni kuhakikisha maslahi ya wananchi yanalindwa.

Mbunge wa Ubungo (CCM), Prof. Kitila Mkumbo, aliyekuwa mwanazuoni wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) taaluma ya elimu, aliutetea mkataba huo unaohusu Bandari, unaruhusu makubaliano pale watakaposhindwa. Alisisitiza kwamba katika awamu ya kwanza ya uwekezaji, DP World itapewa kuendesha gati 0 hadi 7; na kwamba kampuni hiyo ikifanya vizuri itaongezwa maeneo mengine zaidi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Media Brains, Jesse Kwayu, alisema mjadala wa jana ni mwanzo wa mijadala mingine mingi ukiwamo wa kujiandaa na uchaguzi wa serikali za mitaa mwakani na Uchaguzi Mkuu wa 2025.

Alisema Watanzania watapata nafasi ya kujadili mambo yanayowahusu kwa kirefu na kutoa maoni yatakayojenga.

**Lissu**

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu,

Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, alisema suala la muda wa mkataba ambalo limekuwa likipigiwa kelele na wadau mbalimbali, hajaona popote katika pakizungumzwa muda wa ukomo wa mkataba huo.

***Imeandikwa na Restuta James na Enock Charles**

IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
(COMMERCIAL DIVISION)
AT DAR ES SALAAM
COMMERCIAL CAUSE 48 OF 2022
IN THE MATTER OF THE COMPANIES ACT NO 12 OF 2002
AND
IN THE MATTER OF AN APPLICATION MADE UNDER SECTION 281 (1) (a)(ii) OF THE COMPANIES ACT NO 12 OF 2002
AND
IN THE MATTER OF COMPULSORY WINDING UP OF AZURE BOUTIQUE RESORT LIMITED
AND
IN THE MATTER OF PETITION FOR UNFAIR PREJUDICE
BY
STEFANO CIOCCA....................................PETITIONER
VERSUS
AZURE BOUTIQUE RESORT LIMITED..................1ST RESPONDENT
MAX JUENTGEN.....................................................2ND RESPONDENT
AHM HOTEL MANAGER.....................................3RD RESPONDENT
ANATORIA MKARUTAZIA ZACHARIA................4TH RESPONDENT

**THAT, AZURE BOUTIQUE RESORT LIMITED** with Incorporation No. 138047423 Having their registered offices in Mwai Kibaki Road near White Sands Hotel, Dar es salaam, is intended to be wound up.
That on the 22nd December 2022, STEFANO CIOCCA of Mwai Kibaki Road near White Sands Hotel, Dar es salaam has petitioned to the Court praying for an Order under the Companies Act Cap 212 to wind up AZURE BOUTIQUE RESORT LIMITED and appointment of an official liquidator.
The petition will be heard at the HIGH COURT OF TANZANIA, COMMERCIAL DIVISION at DAR ES SALAAM on the 26th day of JUNE, 2023 at 09:30 AM before Hon. MBANGWA-Judge and Address of the Petitioner are under the care of;
**SHALOM SAMWEL MSAKYI, ADVOCATE,**
**LIOR ATTORNEYS,**
**2ND FLOOR, RAHA TOWERS, MAKTABA SQUARE,**
**P.O. Box 7566, DAR ES SALAAM.**
**THEREFORE:** Any person intending to show cause why the prayer of the Petition should not be granted or wishing to appear at the Hearing whether not be granted or wishing to appear at the hearing whether to defend, oppose or in support of this Petition must give Notice of this intention in accordance with the provisions of THE COMPANIES ACT and THE COMPANIES (INSOLVENCY) RULES.

**Dated this 13th day of June, 2023**
**SHALOM SAMWEL MSAKYI**
**Advocate for the Petitioner.**

# Wanafunzi Sudan wahamia Muhimbili kumalizia masomo

**Na Romana Mallya**

WANAFUNZI 150 wa udaktari kutoka Chuo Kikuu cha Tiba, Sayansi na Teknolojia (UMST) cha Khartoum nchini Sudan, wamehamishiwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) ili kukamilisha mwaka wao wa mwisho wa masomo, kutokana na hali ya mapigano yanayoendelea nchini kwao.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa kuwakaribisha wanafunzi hao jana mkoani Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa Muhimbili, Prof. Mohamed Janabi, alisema kuwa mapigano ya nchini humo yamesababisha kufungwa kwa vyuo na baadhi ya shughuli kusimama na kusababisha wataalamu hao kushindwa kuendelea na ratiba zao za masomo ya kawaida.

Prof. Janab alisema wanafunzi hao wapo mwaka wa tano wa Shahada ya Kwanza ya Utabibu na katika mwaka huo, mafunzo hufanyika kwa vitendo zaidi.

"Madaktari hawa wanafunzi watafanya mzunguko (rotation) katika idara mbalimbali ikiwamo ya upasuaji chini ya usimamizi wa madaktari bingwa ili kuhakikisha wanapata maarifa yanayotakiwa," alisema Prof. Janabi.

Alisema kuwa MNH itatoa fursa kwa wataalamu hao kujifunza kama inavyotoa kwa wengine wa ndani na nje ya nchi na baada ya kumaliza masomo kama watapenda kufanya mafunzo tarajali (internship), MNH itawapa nafasi hiyo.

Makamu Mkuu wa Chuo cha UMST, Prof. Mamoun Homeida, alisema, amefurahi kuona wanafunzi kutoka chuo anachokisimamia wamepokewa vizuri na jambo hilo limetokana na uhusiano wa kindugu baina ya Tanzania na Sudan.

Ruba Anwar Salih ambaye ni kiongozi wa kundi la wanafunzi hao akizungumza kwa niaba ya wenzake alisema, wamefurahi kupata fursa ya kuendelea na masomo katika hospitali kubwa ya Muhimbili yenye wataalamu wa kutosha.

Alisema ni imani yao kwamba, wakati wote watakapokuwa hospitalini hapo watapata fursa nzuri ya kujifunza.

# Chongolo abeba kilio cha waziri kumfikishia waziri

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, amesema Wilaya ya Kondoa mkoani Dodoma inakabiliwa na uhaba wa chakula kwa mwaka huu kutokana na mvua zilizonyesha kuwa chini ya kiwango na kuiomba serikali kuwapatia wananchi wake chakula cha msaada.

Dk. Ashatu ambaye ni Mbunge wa Kondoa, aliwasilisha kilio hicho jana katika Kijiji cha Itaswi, Wilaya ya Kondoa mbele ya Katibu wa Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo aliyeko katika ziara ya kikazi kukagua utekelezaji wa Ilani ya chama hicho mkoani Dodoma.

Alisema mwaka huu wanakabiliwa na uhaba wa chakula kutokana na mvua kunyesha chini ya kiwango na kusababisha wananchi kukosa chakula, hivyo wanaiomba serikali kuwasaidia chakula.

"Ndugu Katibu Mkuu wa CCM, wananchi hawa unaowaona hapa wana njaa sana, wanahitaji chakula cha bure kwa sababu walikuwa wanategemea mazao hayo kuuza ili kupata fedha za mahitaji," alisema.



Dk. Ashatu alisema sehemu kubwa ya vijiji vya wilaya hiyo vinakabiliwa na uhaba wa chakula na hali hiyo haijawahi kutokea, hivyo imewapa shaka wananchi wa maeneo hayo.

Mmoja wa wakazi wa Kijiji cha Itaswi, Abedi Duru, alitaja vikwazo vinavyowakabili wananchi ni kukauka kwa Bwawa la Itaswi ambalo lilikuwa liktumika kuvua samaki pamoja na kufanya shughuli za kilimo katika eneo hilo.

Alitaja tatizo lingine kuwa ni mgogoro wa ardhi wa miaka mingi kati ya vijiji vya wilaya hiyo vinavyopakana na hifadhi ya Pori Tengefu la Mkungunero.

Alisema mipaka hiyo imekuwa ikibadilika na kusababisha wananchi kupata usumbufu wa kuvamiwa na askari katika maeneo yao ya asili wanayoishi huku mazao yakiharibiwa.

Alitaja matatizo mengine ni uharibifu wa mazao unaofanywa na wanyamapori wanaotoka kwenye pori hilo na kusababisha hasara ya mazao wanayolima, pia wanyama husababisha vifo na majeruhi kwa baadhi ya wananchi.

Katibu Mkuu wa CCM, Chongolo, alisema atawailisha hoja ya uhaba wa chakula kwa Waziri wa Kilimo, ili kuangalia namna ya kuwasaidia chakula cha bei nafuu au cha msaada.

Chongolo aliwaomba wafanyabiashara wa mazao wa maeneo hayo kutafuta mahindi ya bei nafuu ili kuwauzia wananchi kwa bei nafuu.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS,**
**MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA**
**MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA VIFAA CHAKAVU

Wananchi wote mnatangaziwa kuwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) itauza kwa njia ya mnada wa hadhara wa vifaa chakavu yakiwemo magari, samani za ofisi pamoja na vifaa vingine siku ya Jumanne tarehe 27 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dar es Salaam na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.

Wananchi wote watakaoshiriki mnada huo wanaombwa kufika siku ya Jumapili tarehe 25 Juni, 2023 katika Jengo la UTUMISHI Kivukoni Dar es Salaam kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo ambavyo ni viti vya ofisini "Office Chairs", "Printers" na "Laptops" na siku ya Jumanne tarehe 27 Juni, 2023 kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni katika Ofisi za e-GA Mji wa Serikali Mtumba Dodoma kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo, ambapo pamoja na vifaa vingine, magari yote yameegeshwa katika ofisi za e-GA.

**Maelezo zaidi ya magari hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali:**

| Na | Aina | Modeli | Namba ya Usajili | Mahali lilipo | Hali ya Gari |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | TOYOTA station wagon Diesel Engine | LAND CRUISER V8 | STL2039 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |
| 2 | Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine, | PAJERO ST WAGON | STL2011 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |
| 3 | Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine | PAJERO ST WAGON | STL2010 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Magari hayajalipiwa ushuru na kodi ya ongezeko la thamani (VAT), hivyo Mnunuzi atatakiwa kulipa ushuru na kodi zingine kabla ya kulichukua toka Mamlaka ya Serikali Mtandao
2. Magari yatauzwa kama yalivyo mahali yalipo
3. Mnunuzi wa gari atalazimika kulipa papo hapo amana "deposit" isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya gari na atakamilisha malipo yote ndani ya muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hilo atakosa haki zote za ununuzi wa gari na amana iliyolipwa haitarudishwa.
4. Mnunuzi wa gari atatakiwa kuondosha au kuchukua gari ndani ya muda wa siku saba (07) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
5. Ruhusa ya kuangalia gari itatolewa kwa siku mbili (02) kabla ya tarehe ya mnada husika.
6. Kwa Mnunuzi wa vifaa vingine atatakiwa kulipia kifaa alichopata baada tu ya kumtangaza dalali kuwa mshindi (on fall of the hammer). Kifaa ambacho hakijalipiwa kitanadiwa upya. Pia mnunuzi atakiwa kuchukua kifaa alichonunua papo hapo mara tu baada ya kulipia (cash and carry)
7. Mnada utaanza saa nne (4:00) asubuhi siku ya Jumanne tarehe 27 Juni katika ofisi zake za Dar es Salaam, 2023 na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)**

Mji wa Serikali, Mtaa wa Mtandao, S. L. P. 2833, Dodoma, Simu: +255222129868, Nukushi: +255222129878,
Barua Pepe: info@ega.go.tz, Mkurugenzi Mkuu: dg@ega.go.tz, Tovuti: www.ega.go.tz
"Uadilifu na Ubunifu kwa Utoaji Huduma Bora kwa Umma"



Compassion in Jesus' name

## Procurement Opportunities

### Advertisement for Pre-Qualification of Suppliers and Service Providers

Compassion International Tanzania (CIT) is part of Compassion International, Inc.-the worldwide Christian nongovernmental organization dedicated to child development and advocacy. CIT begun its operation in 1999. Twenty (20) years after the start, we have grown into one of the largest Christian child-focused, advocacy and development organizations in Tanzania. We are a child ministry pairing compassionate people with children living in extreme poverty to release the children from spiritual, economic, social, and physical poverty. In Tanzania Compassion International operates in 21 regions with its Head office in Arusha. CIT is inviting all interested suppliers across Tanzania to express their interest to supply and provide services to CIT as per description below: -

| | |
|---|---|
| Tender No: | PQ/CIT/001-2023 |
| Tender Name | Invitation for Pre-Qualification |
| Reference Number | CATEGORY A: SUPPLY OF GOODS |
| PQ/Goods/ CIT-001 | Supply of Office stationery. |
| PQ/Goods/ CIT-002 | Supply, repair and Maintenance of Electronics and Home Appliances |
| PQ/Goods/ CIT-003 | Supply and maintenance of ICT equipment ie. Photocopier, printer, UPS, etc. |
| PQ/Goods/ CIT-004 | Supply of branded items and promotional materials. |
| PQ/Goods/ CIT-005 | Supply, installation and maintenance of fire and security equipment and systems. |
| PQ/Goods/ CIT-006 | Supply of medicines for First Aids |
| PQ/Goods/ CIT-007 | Supply of office furniture and fixtures. |
| PQ/Goods/ CIT-008 | Supply of office upkeep i.e., tea bags, sugar, etc. |
| PQ/Goods/ CIT-009 | Supply of vehicles |
| PQ/Goods/ CIT-010 | Supply of News papers |
| PQ/Goods/CIT-011 | Supply and Servicing of Music Instrument |
| Reference Number | CATEGORY B: PROVISION OF SERVICES |
| PQ/Service/ CIT-001 | Provision of catering services (Arusha, Mwanza, Dodoma and Dar es Salaam offices) |
| PQ/Service/ CIT-002 | Provision of airtime (Mobile Voice & Data services) |
| PQ/Service/ CIT-003 | Provision of Air travel, reservations, and ticketing services. |
| PQ/Service/ CIT-004 | Provision of fumigation and pest control services. |
| PQ/Service/ CIT-005 | Provision of internet services. |
| PQ/Service/ CIT-006 | Provision of hotel accommodation and conference facilities. |
| PQ/Service/ CIT-007 | Provision of security services (guards) |
| PQ/Service/ CIT-008 | Provision of repair and maintenance of vehicles, motorcycles, and generators |
| PQ/Service/ CIT-009 | Provision of Building Repair & Maintenance Service (painting, plumbing, electrical etc.) |
| PQ/Service/ CIT-010 | Provision of Courier service |
| PQ/Service/ CIT-011 | Provision of Chartered plane service |
| PQ/Service/ CIT-012 | Provision of Translation Services |
| PQ/Service/ CIT-013 | Provision of Cleaning & Gardening services |
| PQ/Service/ CIT-014 | Provision of vehicle Tracking Services |
| PQ/Service/ CIT-015 | Provision of Vehicle Hire service |
| PQ/Service/ CIT-016 | Provision of printing services |
| PQ/Service/CIT-017 | Provision of Vehicle Insurance Service |
| PQ/Service/CIT-018 | Provision of part time staff for Data collection, Data Entry, drivers, receptionist etc. |
| PQ/Service/CIT-019 | Provision of video and photography services |
| PQ/Service/CIT-020 | Provision of TV and radio program airing services |
| Eligible Firms | National (Registered in Tanzania) |
| Method of Procurement | National Competitive Bidding |
| Mandatory Documents for submission | - Business License<br>- TRA documents (TIN/VRN certificate and Tax Clearance, proof of EFD)<br>- Regulatory body documents if applicable (TBS, TFDA, TMDA, TIRA, etc.)<br>- Registration/incorporation Certificate if applicable (BLERA)<br>- Company Profile (Among other things, state your coverage in Tanzania)<br>- Price list, delivery terms and payment terms.<br>- Evidence of similar work experience (Contract/Purchase orders)<br>- Business bank details (Acc name, number, bank name, providing bank statement is an added advantage)<br>- Official business address (Physical, post, email and phone number) |
| Mode of Application (Soft Copy) | Via Email, tzprocurement@tz.ci.org<br>Please send all your documents in a single PDF file, indicate in your document and on the subject of your email, the category you are applying for; Your documents must be signed & stamped |
| Mode of Application (Hardcopy) | Olorien, Mtoto House, Plot No.18, P.O. Box 3064, Arusha Tanzania.<br>Pack your documents into a sealed envelope; your documents must be signed & stamped |
| Bids Submission | Effective 19th June 2023 to 06th July 2023 |

# DCEA yatoa hadhari uhusiano kimapenzi na raia wa kigeni

**Na Gwamaka Alipipi**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) imetahadharisha kutumika mbinu mpya za wafanyabiashara wa dawa za kulevya hususani raia wa kigeni, ikiwamo ya kuwatumia wanawake wa kitanzania kusafirisha dawa hizo na kuwaweka matatani.

Imesema raia hao wa kigeni huanzisha uhusiano wa kimapenzi na wanawake wa kitanzania zaidi ya mmoja, kisha wanawatumia kusafirisha dawa za kulevya au kuzihifadhi katika nyumba zao.

Kamishna Jenerali wa mamkala hiyo, Aretas Lyimo, alitoa hadhari hiyo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu operesheni ya ukamataji wa dawa za kulevya waliyoifanya katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Kilimanjaro na Arusha kwa miezi mitatu.

Alisema katika operesheni hiyo, kilogramu 200.5 za dawa za kulevya aina ya heroin, cocaine kete 138 na methamphetamine gramu 531.4 zilikamatwa.

Alisema mbali na dawa hizo, pia zilikamatwa kilo 1.5 za bangi iliyosindikwa, magunia 978 ya bangi kavu, magunia 5,465 ya bangi mbichi na ekari 1,093 za mashamba ya bangi yaliteketezwa.

Pia alisema kuwa kupitia operesheni hiyo, walikamata milimita 3,840 za dawa tiba zenye asili ya kulevya aina ya pethidine.

Kamishna Jenerali huyo alisema DCEA kwa kushirikiana na Bodi ya Kimataifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya (INCB) ilizuia kuingia nchini kilo 1,507.46 za kemikali bashirifu ambazo zingeweza kutumika kutengeneza dawa za kulevya.

"Kutokana na udhibiti mkubwa, wafanyabiashara hawa wamebuni mbinu mpya hasa raia wa kigeni kuanzisha uhusiano wa kimapenzi na wanawake wa kitanzania.

"Niwatahadharishe wanawake wasikubali kuanzisha uhusiano na watu wasiowafahamu, huwa wanawatumia mbinu hii kusafirisha dawa za kulevya au kuzihifadhi katika nyumba zao. Tunapowakamata mzigo, unakutwa kwa mwanamke na yule mwanamume anamkana kabisa. "Ninapenda kutoa rai kwa Watanzania wote hususani wanawake wa kitanzania, kuwa makini pindi wanapopewa mizigo na watu bila ya kujua ndani kuna kitu gani.

"Zaidi, ninatoa tahadhari kwa wanawake wanaoanzisha uhusiano wa kimapenzi na raia wa kigeni! Kwani katika kesi nyingi tulizonazo hivi sasa zinawahusu moja kwa moja wanawake," alionya.

Kamishna Jenerali Lyimo alibainisha kuwa kuanzia Machi 25 hadi Juni 19 mwaka huu, wamekamata watuhumiwa 109, wakiwamo raia wa kigeni watatu.

"Mwanamke anakatwa nyumbani kwake akiwa na mzigo wa dawa za kulevya, lakini hadi anakamatwa alikuwa hajui mzigo huo ulikuwa wa nini! Anasema alipewa tu na mpenzi wake amhifadhie."

Lyimo alisema kuwa hali hiyo imesababisha wanawake wengi wa kitanzania kujikuta wakiingia katika matatizo ya kukamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.




Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo TIB, Lilian Mbassy (kulia), akimkabidhi vifaa vya kufanyia usafi Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo, Voster Mgina (kushoto), wakati watumishi wa TIB walipofanya usafi katika kituo cha mabasi SIMU 2000 ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma kwa mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wosia aliyejikata shingo kwa mashine ya mbao watekelezwa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MWILI wa Mwita Warioba (40), anayedaiwa kujiua kwa kutumia mashine ya kuchania mbao, ulisafirishwa jana kwenda Musoma mkoani Mara kwa ajili ya maziko.

Mwili huo umesafirishwa baada ya 'tajiri' aliyetajwa na marehemu kwenye ujumbe alioacha, kutii wito wa kutakiwa kuusafirisha mwili huo, la sivyo 'atakuwa anamtokea na kumsumbua kila mara'.

Warioba alidaiwa kujiua asubuhi ya Juni 16, mwaka huu katika Mtaa wa Rau, Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro, akiwa kwenye kiwanda cha mbao.

Akizungumzia mkasa huo na namna mmiliki wa kiwanda hicho, Erasto alivyotii wosia ulioachwa na mfanyakazi wake, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Karikacha, Sweetfrid Malewo alisema:

"Ni kweli mwili ulisafirishwa jana (juzi). Tuliuaga pale KCMC (Hospitali ya Rufani ya Kanda), baada ya kikao cha juzi cha familia ya marehemu kukaa na upande wa kina Erasto (mwajiri wake).

"Walijiridhisha kwamba tukio lile ni kweli ndugu yao ameamua mwenyewe kujiondoa uhai wake, lakini halihusiani kwa chochote na mwajiri wake.

"Baada ya kile kikao, walikuja na majibu wakasema wao watakwenda kama watu wanane tu, kwa hiyo wakipatiwa basi dogo aina ya Hiace au Landcruiser lingewatosha kuwapeleka wao na mwili wa marehemu mpaka huko kwao Musoma, Mara."

Malewo aliiambia Nipashe kuwa tajiri huyo alikubaliana na familia ya marehemu kugharamia kuusafirisha mwili na kulipa gharama za chakula msibani.

"Mwili uliondoka jana (juzi) kwa kutumia Hiace na Erasto amelipa Sh. milioni 1.8 kuupeleka mwili mpaka kijijini atakapozikwa marehemu Warioba.

"Kulitokea ubishani pale, mama yake akasema kama hatogharamia chakula, ni bora huo mwili ubaki hukuhuku (Moshi).

"Lakini Erasto, akaamua kulibeba jambo hilo na kulipa fedha ya chakula Sh. 500,000, ndipo wakakubali kuubeba mwili na tukawaaga kwa sala," alisema Malewo.

Taarifa iliyotolewa na Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi, Yahya Mdogo, inaeleza kuwa kabla ya kifo chake, Warioba alikuwa amesimamishwa kazi kwa tuhuma za wizi wa fedha za mapato za karakana hiyo na kutakiwa kutoa ufafanuzi kuhusu fedha hizo.

Kamanda Mdogo alisema katika taarifa yake: "...aliamua kuchukua hatua hiyo ya kujikata shingo kwenye mashine inayozungushwa kwa umeme, kwa makusudi na kuacha ujumbe kabla hajajiua kuwa ameamua kwa hiari yake kujiua."

# Jenerali Mkunda ataka majeshi kuliwakilisha vyema taifa

**Na Mwandishi wa Maelezo,** RWANDA

MKUU wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Jacob Mkunda, amevitaka vikosi vya ulinzi na usalama nchini vinavyoshiriki zoezi la Ushirikiano Imara 2023 kwa majeshi ya nchi za Afrika Mashariki, kuliwakilisha vyema taifa ili kujenga ushirikiano mzuri na nchi jirani.

Akizungumza baada ya ufunguzi wa zoezi linalofanyika mji wa Musanze, Rwanda, Jenerali Mkunda alisema kuna haja ya zoezi hilo liwe chachu ya kujifunza namna ya kutatua changamoto za kiulinzi na usalama katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuwa wananchi wanayategemea zaidi majeshi yao kuwapatia msaada wa ulinzi na uokozi majanga yanapotokea.

"Unajua hakuna kitu kikubwa ambacho huwa kinarudisha na kujenga imani ya wananchi kwa majeshi yao kama kupewa msaada wa kijamii pindi wapatapo majanga. Imani yao kubwa hubaki kwa wanajeshi ambao ndio huwa wa kwanza kutoa msaada," alisema Jenerali Mkunda.

Pia avitaka vikundi vinavyoshiriki zoezi la Ushirikiano Imara 2023 kudumisha udugu na ushirikiano wa majeshi kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

"Nchi yetu ya Tanzania kwa muda mrefu imekuwa ikisifika kwa kuwa marafiki wa kweli katika nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na dunia nzima, hivyo hakikisheni mnaendelea kuwa mfano wa kuigwa," alisisitiza Jenerali Mkunda.

Akizungumzia umuhimu wa ushirikishwaji wa zoezi hilo kwa taasisi na mamlaka za kiraia, Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema huu ni wakati mwafaka wa kufanya kazi pamoja kwa kuwa majanga yanapotokea, mamlaka mbalimbali zinahusika kutoa utaalamu wa kukabiliana na majanga hayo.

"Tupo tayari kufanya kazi na majeshi ya ulinzi na usalama kuhakikisha tunatekeleza majukumu yetu ya kihabari kusaidia kufanikisha majukumu ya kulinda amani na kurudisha imani ya wananchi pale majanga yanapotokea," alisema Msigwa.

Zoezi hilo la wiki mbili lilifunguliwa rasmi juzi na Waziri wa Ulinzi wa Rwanda, Juvenal Marizamunda, ambaye alimkabidhi bendera ya kuashiria kuanza kwa zoezi hilo.

Mkuu wa zoezi hilo, Dk. Alice Urusaro Uwagaga Karekezi, alikabidhi bendera hiyo kwa Mkuu wa Majeshi ya Kikanda (REMIKA), Brigedia Jenerali Julius Gambosi.

Zoezi linalenga kuvijengea vikundi vya ulinzi na usalama pamoja na taasisi za kiraia uwezo wa kukabiliana na ugaidi, uharamia, menejimenti ya majanga pamoja na ulinzi wa amani katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Washiriki wa zoezi hilo ni pamoja na majeshi ya ulinzi, Polisi, Magereza, Uhamiaji, Zimamoto na Kituo cha Taifa cha Kukabiliana na Ugaidi.

Taasisi za kiraia zilizoshirikishwa ni pamoja na zilizo chini ya sekta za habari, haki za binadamu, usawa wa kijinsia pamoja na diplomasia na ushirikiano wa kimataifa kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

## HABARI KITAIFA

# Ajali ya basi, lori ilivyoua, kujeruhi

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

YOHANA Mwamlima (40), mkazi wa Temeke, amefariki dunia huku watu wengine wanane wakijeruhiwa katika ajali iliyohusisha lori la mafuta na basi barabara ya Morogoro.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani Morogoro, Emmanuel Ocheng, akizungumza na waandishi wa habari katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, alisema ajali hiyo ilitokea saa tano usiku wa kuamkia jana eneo la Kingolwira mkoani hapa.

Alisema ajali hiyo ilihusisha gari aina ya Howo lenye namba za usajili T 690 DSV /T 800 DSV lililokuwa linatoka Dar es Salaam.

Kamanda huyo alisema gari hilo lililokuwa linaendeshwa na Nkandi Konokwa (61), mkazi wa Nzega mkoani Tabora, liligonga basi lenye namba za usajili T 728 EBT lililokuwa linatokea Musoma kwenda Dar es Salaam, likiendeshwa na Ahmed Salum (32), mkazi wa Mwanza.

Mratibu wa Tiba na Utafiti wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, Dk. Abdilah Issa, alithibitisha kupokea mwili wa marehemu na majeruhi wanane usiku wa kuamkia jana. Majeruhi watano ni wanaume na watatu ni wanawake.

Dk. Issa ambaye ni Kaimu Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, alisema mmoja wa majeruhi wanaume hali haikuwa nzuri. Madaktari walikuwa wanaendelea na jitihada za matibabu kwa ajili yake na wagonjwa wengine.

Kwa mujibu wa mmoja wa majeruhi waliolazwa katika hospitali hiyo, Vaileth Joseph aliyekuwa anatoka Musoma kwenda Dar es Salaam, alisema kuwa akiwa katika gari hilo, alihisi basi linakwenda mwendo kasi na ndipo akaamua kufunga mkanda na kulala na aliposhtuka ndipo akabaini basi limeshaanguka huku akiwa ameumia sehemu za mbavu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Alex Mkama, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo. Wanamshikilia dereva wa gari lililosababisha ajali, Nkandi Konokwa.

Kamanda Mkama alisema majeruhi watano kati ya wanane walitibiwa na kuruhusiwa. Watatu waliokuwa katika basi, walikuwa wanaendelea na matibabu hospitalini. Aliwataja majeruhi hao kuwa ni: Onesmo Malegesi (35), mkazi wa Lindi; Anastazia Manyerere (19), mkazi wa Musoma; na John Ngewe (25), mkazi wa Kibaha.

Kamanda Mkama alisema chanzo cha ajali hiyo ni dereva Konokwa kuhamisha gari kutoka upande wake wa kushoto na kwenda kulia bila tahadhari na kusababisha ajali hiyo.

Kufuatia kutokea ajali mfululizo katika barabara kuu zinazoenda mikoa na nchi jirani mkoani hapa, Kamanda Mkama alisema jeshi hilo linaendelea na doria kupunguza au kukomesha ajali huku akiwataka madereva kuzingatia mafunzo wanayopata na kuheshimu maadili na viapo vya kazi zao. Kutasaidia kuepuka ajali za barabarani.

# 'Waajiri wabanwe uwasilishaji michango mifuko hifadhi jamii'

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

BUNGE limeitaka serikali kuwabana waajiri wasiopeleka michango ya wafanyakazi wao katika mifuko ya hifadhi ya jamii kutokana na kuwasababishia kusotea mafao pindi wanapostaafu.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Akson, alitoa maelekezo hayo jana bungeni baada ya wabunge wengi kulalamikia wastaafu kusotea mafao.

Dk. Tulia alisema wastaafu wamekuwa wakipata kero wanapofuatilia mafao yao kutokana na waajiri kutopeleka michango, jambo ambalo limekuwa kero kubwa kwa wapigakura.

"Pamoja na jitihada zinazofanywa, wastaafu wanapokwenda huko kwenye mifuko badala ya kuwalipa fedha unawaambia kafuatilie mwajiri wako kule wakati kazi ya kufuatilia siyo ya mwajiriwa, kwa sababu yeye hawezi kuuliza kama umepeleka au hujapeleka.

"Tunashindwa kuelewa ile ni kazi ya yule mwenye mfuko ama ni kazi ya mfuko kufuatilia kwa yule ambaye halipi. Ninadhani hilo mwendelee kulifuatilia upande wa mifuko. Je, waajiri wanapeleka?

"Kama hawapeleki, ichukulieni hatua mifuko lakini huyu mwajiriwa asipate tabu. Anapostaafu, alipwe fedha yake," aliagiza.

Akitolea ufafanuzi kuhusu suala hilo, Naibu Waziri Ofisi ya Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, aliwaagiza mameneja wa mifuko ya hifadhi ya jamii wa mikoa kuhakikisha hakuna malalamiko ya wastaafu katika maeneo yao kwa kuwa hicho ndicho kitakuwa kipimo cha utendaji kazi wao.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Angelina Malembeka, alitaka kujua mpango wa serikali kulipa wastaafu ambao hawajapata mafao yao wakiwamo wafanyakazi wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) na hatua zilizochukuliwa kwa waajiri wasiopeleka mafao ya watumishi katika mifuko.

Katambi alisema taarifa zilizopo ofisini zinaonyesha wameshalipwa zaidi ya wafanyakazi 500 na wamebaki wachache ambao hawajawasilisha nyaraka na taarifa sahihi.

Kuhusu hatua zinazochukuliwa kwa waajiri wasiowasilisha mchango wa waajiriwa kwa wakati, Katambi alisema mifuko ina sheria zinazoelekeza kuwa ni kosa kwa mwajiri kutokuwasilisha michango kwa wakati katika mifuko.

Mbunge wa Kigamboni (CCM), Dk. Faustine Ndugulile, alisema wastaafu wengi wanapata adha ya kufanya uhakiki wa mara kwa mara kuthibitisha.

"Je, ni mkakati gani serikali itachukua hatua kuhakikisha kwamba kunakuwa na mfuko wa kisasa wa kufanya uhakiki badala ya kuwapo usumbufu ambao upo hivi sasa?" Dk. Ndugulile alihoji.

Akijibu swali hilo, Katambi alisema kutokana na tatizo hilo kwa sasa huduma zinapatikana kwa mfumo wa TEHAMA na wanapewa huduma vizuri.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka 2020/21 inazitaja Halmashauri za Jiji la Dodoma na Nzega zinaongoza kwa kutowasilisha michango ya watumishi katika mifuko ya hifadhi ya jamii.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI**

DISTRICT COUNCIL IKUNGI

S.L.P 42
SINGIDA

# TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**TAREHE: 20-06-2023**

Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi anawatagazia wananchi wote nchini Tanzania, kuwa kutakuwa na mnada wa hadhara wa kuuza magari chakavu manne (04) kwa njia ya mnada wa hadhara tarehe **05/07/2023**

**Magari yanayopigwa mnada ni kama yanavyoonekana kwenye jedwali hapo chini;**

| S/N | REG NO. | MODEL | ENGINE | CHASES |
|---|---|---|---|---|
| 01 | SM 3293 | ISUZU FSR | 6HH1- 301622 | JALFSR33HW3000221 |
| 02 | SM 3194 | TOYOTA L/ CRUISER H/TOP-scrap | IHZ- 0412122 | JTERB71J500010214 |
| 03 | SM 4591 | TOYOTA HILUX D/C | 5L- 5630294 | AHTFK22GX03003435 |
| 04 | STJ9159 | TOYOTA/CRUISER H/TOP | IHZ- 0392775 | JTERB71J700013504 |

**MASHARTI YA MNADA**


1. Gari /kifaa kitauzwa kama kilivyo mahali kilipo
2. Mnunuzi atalazimika kulipa papo hapo amana (deposit) isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya gari /kifaa alichonunua na kukamilisha malipo yote katika muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hilo atakosa haki zote za ununuzi wa kifaa/grari husika na amana aliyolipa awali haitorudishwa.
3. Mtu yeyote atakayetangazwa kuwa mshindi na akashindwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya bei ya gari siku ya mnada atachukuliwa kuwa anavuruga utaratibu wa mnada na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.
4. Mnunuzi atatakiwa kuondoa au kuchukua kifaa/ gari alilonunua katika muda wa siku saba (07) kuanzia siku ya kukamilisha malipo. Aidha, mnunuzi atatakiwa kubadili umiliki wa gari alilonunua katika muda wa siku thelathini (30).
5. Mshindi wa mnada atakuwa na jukumu la kufanya malipo yote ya tozo na kodi kuhusiana na gari alilonunua.
6. Ruhusa ya kuangalia na kukagua vifaa na magari itakuwa katika muda wa kazi kuanzia saa tatu asubuhi mpaka saa tisa alasiri (3:00 – 9:00) siku ya Jumatano tarehe 28/06/2023 hadi siku ya Alhamis Tarehe 04/07/2023 katika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya Ikungi kama ilivyoorodheshwa.
7. Mnada utaanza saa nne kamili (4:00) asubuhi siku ya Jumatano tarehe 05/07/2023 kwa magari yote yaliyoko ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi.

**LIMETOLEWA NA:**

.............................
**JUSTICE L. KIJAZI**

**MKURUGENZI MTENDAJI,**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII




# Wazazi acheni binti zenu wapate elimu, msikimbilie kuwaoza

**HIVI** karibuni kumetokea tukio la kuvunjwa kwa ndoa kati ya mwanamume mmoja na mwanafunzi kutokana na tamaa ya wazazi kupata pesa na kuamua kumwoza mtoto wao.

Ndoa hiyo ilivunjwa na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, ambaye alishirikiana na wadau wa msaada wa kisheria pamoja na Jeshi la Polisi mkoani humo.

Kwanza juhudi zilizofanywa na kiongozi huyo mpaka kuhakikisha anamwokoa mwanafunzi huyo katika ndoa hiyo ni za kupongezwa.

Mwanafunzi huyo inaelezwa alikuwa amechaguliwa kuingia kidato cha tano, lakini wazazi wake wakamlazimisha kuolewa badala ya kuendelea na masomo.

Tukio hilo la kuvunjwa kwa ndoa lilitokea Ijumaa iliyopita majira ya saa 11 jioni nyumbani kwa wazazi wa mwanafunzi huyo baada ya Mwenyekiti wa Kamati ya Msaada wa Kisheria Mkoa wa Shinyanga, John Shija, kupata taarifa za siri kutoka kwa msamaria mwema kuhusu kuwapo wa ndoa hiyo ambayo ililenga kukatisha ndoto ya masomo ya mtoto huyo.

Mwenyekiti huyo aliamua kuweka mtego na kisha kuwasiliana na Jeshi la Polisi pamoja na Mkuu wa Mkoa ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama na wote kwa pamoja kuvamia harusi hiyo na kuwakamata wahusika huku wazazi wao wakikimbia.

Kwa mujibu wa mwenyekiti, taarifa walizozipata ni kuwa mtoto huyo amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano, Urambo mkoani Tabora, lakini wazazi wake hawakutaka aendelea na masomo badala yake wakamlazimisha aolewe ili wapate mali.

Ni watoto wangapi wanaopitia kadhia hiyo kutoka kwa wazazi wao na taarifa kutowafikia wahusika? Hii inaonesha bado kuna wazazi wenye mawazo finyu ya kukatisha ndoto za mabinti zao za kuendelea na elimu na kuwatumia kama kitega uchumi cha kuwaletea pesa kwa kuwaozesha mapema.

Wengi wa wasichana wanaolazimishwa kuolewa wanapitia mateso makubwa kwa kuwa hawajafikia umri wa kuishi na wanaume na hata viungo vyao vya uzazi havijakomaa kuhimili kupata watoto na kujikuta wakipata kwa njia ya upasuaji na wengine kupata ugonjwa wa fistula.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga katika kukemea kitendo hicho, alisema hayupo tayari kuona watoto wa kike wanashindwa kufikia ndoto zao kwa tamaa ya wazazi wao kutaka kupata mali na kusababisha kuzima ndoto zao.

Amewaonya wazazi wa aina hiyo kuacha watoto wao watimize ndoto zao badala ya kuingia tamaa ya kuwaozesha katika umri mdogo. Ameshauri kama mwanamume anampenda binti ni bora amsubiri hadi amalize Chuo Kikuu ndipo atakuwa na uamuzi mwenyewe wa kuolewa ama la.

Pia wazazi wa mwanafunzi huyo ambao wamekimbia baada ya kutokea tukio hilo, wametakiwa kujisalimisha polisi wenyewe badala ya kusibiri watafutwe.

Serikali katika kuhakikisha binti huyo anapata haki ya msingi ya kupata elimu na kufikia ndoto zake, imeahidi kumsimamia ili atimize ndoto yake ya kuwa na elimu bora huku ikiwaonya wazazi wenye tamaa ya mali kupitia mabinti zao kuacha tabia hiyo kwa kuwa mkono wa sheria unaangaza muda wote.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Kupimwa uwezo kunaweza kuuletea heshima uwalimu

**BAADA** ya Uhuru mwaka 1961 ualimu uliheshimika kama kazi yenye hadhi na heshima zote, walimu walikuwa watu wa maadili, wenye hekima, nadhifu na watanashati, wenye ufahamu mkubwa, wanaoishi maisha bora na pia wanaokubalika na jamii.

Lakini leo mambo yamebadilika ni kuanzia miaka ya 1980 ukaibuka mtazamo wa kuiona taaluma ya ualimu kuwa ni chaguo la mwisho baada ya kukosa njia nyingine ya kupata ajira, kitendo ambacho hata waliopata alama za chini walijiunga na vyuo vya ualimu bila kustahili.

Hata aliyekuwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, wakati huo, Philipo Mulugo aliwahi kukaririwa na vyombo vya habari akisema wanafunzi waliopata daraja la nne na pointi 27 wangechaguliwa kujiunga na vyuo vya ualimu kama wangeomba nafasi hiyo.

Kauli yake ilikuwa ni baada ya wanafunzi wengi waliofanya mtihani wa kidato cha nne mwaka 2012 na kuangukia pua wakipata daraja la nne na kwamba ndio ambao walitarajiwa kujiunga na mafunzo ya cheti katika vyuo vya ualimu mwaka 2013.

Kwa utaratibu huo, elimu ya Tanzania ilikuwa mashakani, kutokana na kwamba waliokwenda katika vyuo vya ualimu kisha kupangwa katika shule mbalimbali mchango wao usingekuwa mkubwa.

Nionavyo, walimu watu muhimu kwa kustawi kwa taifa lolote na kustawi kunatokana na watu kupata elimu bora inayokidhi na kukabiliana na mazingira,

Hivyo, ni wazi kwamba, wanaokwenda katika vyuo vya ualimu wakiwa na ufaulu mzuri, watakuwa na uwezo wa kufanya kazi yao kwa ufanisi ya kuwaandaa wataalamu wa fani mbalimbali wa baadaye.

Hata hivyo, mtazamo wa kuiona taaluma ya ualimu kama chaguo la mwisho baada ya kukosa fursa nyingine, inaendelea kufutika taratibu kutokana na mikakati mbalimbali inayofanywa na Wizara ya Elimu.

Mojawapo ua mikakati hiyo, ni huu uliotangazwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda kwamba, ili mwalimu aajiriwe, atapaswa kufanya mtihani wa kupima uwezo wako.

Anasema utaratibu huo utaanza kufanya kazi, katika ajira mpya za taaluma hiyo, kwamba wakati wa kutangaza nafasi mpya za ualimu, watakaotaka kupata kazi, watafanya mtihani hata kama wamesoma.

Kwa mujibu wa waziri huyo ni kwamba, baada ya kufanya mtihani, wataona matokeo, wataangalia idadi ya walimu inayohitajika, kisha watachukua waliofaulu na kuwaajiri.

Hapa kinachotafutwa ni wizara hiyo, ni kurudisha hadhi ya taaluma ya ualimu, ili isitazamwe kuwa chaguo la mwisho baada ya kukosa fursa nyingine za ajira kama ambavyo imezoeleka.

Utaratibu wa kupeleka vyuo vya ualimu wanafunzi waliofeli, ulishafutika, kwani nchi ingeendelea kuzalisha wanafunzi wenye matokeo mabaya.

Lakini utaratibu mpya wa ajira kwa walimu ambao umetengezwa na waziri, ni wazi utasaidia kuwachuja na kupata wale ambao wanaweza kufanya kazi vizuri, hasa kwa kuzingatia kwamba ualimu ni wito.

Ninaipongeza wizara kwa kuja na utaratibu huo wa ajira, kwani inawezekana wakawamo waliopita vyuoni, lakini wakawa hana uwezo wa kufikia kile ambacho serikali inakitaka kwenye elimu.

Pamoja na hayo, imekuwa ni kawaida kwa wanafunzi waliopata madaraja ya kwanza na ya pili, kukataa kujiunga na vyuo vya ualimu kwa maelezo kwamba kazi ya ualimu ina maslahi duni.

Hivyo, wakati serikali inakutana na mikakati ya kuboresha elimu, ingekuwa ni nafasi nzuri ya kuangalia maslahi hayo na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili walimu.

Ikumbukwe kuwa suala la maslahi ya walimu katika shule za umma ndilo ambalo husababisha wengi kukimbilia shule binafsi, kitendo ambacho kwa namna moja au nyingine, kinaweza kukwamisha maendeleo ya elimu.

## Tuzo 70 kuwaniwa 'Consumer Choice Awards Afrika 2023'

**Na Joseph Mwendapole**

KATIKA jitihada za kusaidia walaji kutoa maoni yao kuhusu ubora wa bidhaa na huduma wanazozipata sokoni, tuzo za Consumer Choice Awards Africa (CCAA) mwaka huu zinatarajia kushindanisha kampuni mbalimbali katika aina zaidi ya 70 za tuzo.

Akizungumza katika uzinduzi wa tuzo za mwaka huu, Mkurugenzi Mtendaji wa CCAA, Diana Laizer, alisema mashindano ya mwaka huu yatahusisha aina kuu 22 za tuzo pamoja na nyingine ndogo zaidi ya 70.

Alitaja aina za tuzo zitakazoshindaniwa kuwa ni usafirishaji, mawasiliano ya simu, usafiri wa anga, huduma za kifedha, ujenzi, huduma za bima, mafuta na gesi, hoteli, usalama, bidhaa zinazotoka haraka, matukio na mapambo, mitindo na ubunifu, pamoja na upigaji picha.

"Katika kipindi cha miaka minne iliyopita, tumeweza kufikia maelfu ya wateja barani Afrika kupitia njia ya mtandao na kukusanya maoni yao juu ya bidhaa na huduma wanazotumia na zaidi ya tuzo 70 zimekuwa zikitolewa kila mwaka. Tunajivunia mafanikio haya," alisema.

Akizungumzia mchakato wa kuwapata washindi, Diana alibainisha kuwa hupatikana kupitia utaratibu wa kupiga kura mtandaoni na walaji wana nafasi ya kupigia kura bidhaa au huduma zinazoshindanishwa kupitia tovuti ya CCAA.

"Baada ya kupokea mapendekezo kutoka kwa washiriki katika makundi tofauti, timu yetu inafanya kazi ya kupanga makundi hayo kulingana na mapendekezo na vigezo vya tuzo husika. Zoezi hili likikamilika makundi huwekwa mtandaoni na walaji hupiga kura kulingana machaguo yao. Upigaji kura hufanyika kwa siku zisizopungua 25 na mlaji anaweza kupiga kura mara moja tu katika kila aina ya tuzo," alifafanua.

Kwa mujibu wa Diana, baada ya muda wa kupiga kura kumalizika, mfumo huonyesha matokea kulingana na idadi ya kura ambazo bidhaa au huduma imepigiwa.

"Dirisha la kupendekeza aina za tuzo kwa mwaka 2023 limefunguliwa rasmi kuanzia leo tarehe 18 Juni 2023 na litaendelea hadi tarehe 9 Julai 2023. Zoezi la upigaji kura litatangazwa baadaye mwaka huu, kwahiyo tunayahimiza kampuni na chapa kushiriki na kushirikisha wateja wao," aliongeza.

Mkurugenzi huyo alipongeza kampuni zinazoshiriki na kuwahamasisha wateja wao kuzipigia kura.



Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, akipata maelezo kutoka kwa mjasiriamali, Grace Nacksson, kuhusu unga wa ubuyu ambao unasaidia kuongeza vitamini C unatumika kwenye chai, uji na juisi, katika maonyesho ya Wiki ya Barcode kitaifa 2023 yaliyofanyika Viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wanafunzi 12 vyuo vikuu vitatu waonyesha ujuzi lugha Kichina

**Na Mwandishi Maalum**

WANAFUNZI 12 kutoka vyuo vitatu vya elimu ya juu Tanzania wameonyesha ujuzi wao katika lugha ya Kichina kwenye Mashindano ya 22 ya "Daraja la Lugha ya Kichina", ambayo ni ya umahiri wa Lugha ya Kichina yaliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa Tovuti ya Gazeti la Umma ya China, katika mashindano hayo yaliyoandaliwa na Taasisi ya Confucius (CI) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kushirikiana na Taasisi ya Confucius ya Chuo Kikuu cha Dodoma na Darasa la Confucius la Chuo Kikuu cha Zanzibar, washiriki walipimwa na jopo la majaji.

Majaji hao ni maofisa Wachina kutoka kampuni za kibiashara za China zilizowekeza Tanzania, katika ujuzi wao wa Lugha ya Kichina, ikiwa ni pamoja na kutoa hotuba kwa lugha ya Kichina, ujuzi kuhusu China na maonyesho ya vipaji ambayo yalilenga kuelewa utamaduni wa nchi hiyo.

Pendo Malangwa, Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, aliipongeza Taasisi ya Confucius kwa kufanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha vijana wa Tanzania wanaweza kujifunza lugha hiyo ili kuboresha uwezo wao wa kiushindani katika kujiendeleza kikazi hapo baadaye.

"Kujifunza lugha ya Kichina ni mbinu mwafaka katika kuendeleza uhusiano kati ya China na Afrika," alisema.

Naye Mratibu wa Mafunzo ya Baada ya Shahada ya Kwanza katika Chuo cha Masuala ya Binadamu cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Herbert Ndomba, alisema mashindano hayo yamewapa wanafunzi maarifa kuhusu utamaduni wa China.

"Mashindano haya yanasaidia wanafunzi kuimarisha ujuzi wao wa lugha na mawasiliano, ujuzi huu ni muhimu katika maisha yetu ya kila siku na katika soko la ajira," alisema Ndomba.

Wang Siping, Konsela wa Utamaduni katika Ubalozi wa China nchini Tanzania, amewataka vijana wa Tanzania kujitolea katika urafiki kati ya China na Tanzania, na kuwatia moyo wa kuishi kwa kuendana na wakati.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Confucius ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Zhang Xiaozhen, amesema madhumuni ya kuandaa mashindano hayo ni kuboresha umahiri na kiwango cha wanafunzi wa Tanzania wanaojifunza Lugha ya Kichina, kuhimiza kikamilifu mabadilishano ya kitamaduni na lugha kama njia ya mawasiliano na utamaduni kama daraja na kuchangia kwenye lengo kuu la urafiki na ushirikiano kati ya China na Tanzania.

Everius Gozibeth Rwabangi (23), mwanafunzi wa mwaka wa tatu anayesomea Shahada ya Kwanza ya Sanaa na Elimu (Lugha za Kichina na Kiingereza), aliibuka mshindi wa jumla. "Kujifunza Kichina ni kama ufunguo wa milango kwa fursa kadhaa katika biashara zinazosimamiwa na China nchini Tanzania," alisema.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Wakazi Mbala walalamika kukosa kibali ujenzi zahanati

**Na Julieth Mkireri,** VIGWAZA

WAKAZI wa Kitongoji cha Mbala Kijiweni, Kijiji cha Chamakweza, Kata ya Vigwaza, wamelalamikia kukosekana kwa kibali cha ujenzi wa zahanati kutoka Halmashauri ya Chalinze na kulazimika kutembea umbali wa zaidi ya kilomita 20 kufuata huduma za afya.

Kwa mujibu wa wananchi hao tayari fedha za fundi, eneo na vifaa wanavyo, lakini wamekwama kupata kibali kutoka halmashauri ili ujenzi wa zahanati katika kitongoji chao uanze.

Akizungumza na Nipashe, mmoja wa wazee wa kitongoji hicho, Raisi Sumulek, alisema vipo vifaa kwa ajili ya ujenzi wa zahanati walipatiwa na wafadhili miaka minne iliyopita, lakini vimeshindwa kutumika kutokana na kukosa kibali.

Sumulek alisema vifaa hivyo vimehifadhiwa katika moja ya darasa la Shule ya Msingi Mbala kwa muda mrefu vikisubiri kibali.

Mwenyekiti wa Kitongoji hicho, Lepa Mumbi, alisema kuna zahanati imejengwa katika Kijiji cha Chamakweza, lakini bado ipo mbali na Kitongoji cha Mbala Kijiweni na wanachoomba ni halmashauri kuwapatia kibali waanze ujenzi.

Mumbi alisema wanafuatilia kibali ofisi ya mkurugenzi na kupewa majibu ya kwamba haiwezekani kujenga zahanati mbili katika kijiji kimoja na kusababisha vifaa walivyopewa na wafadhili kuendelea kukaa darasani huku vingine vikiwa hatarini kuharibika.

"Eneo lipo limesafishwa tayari, vifaa vipo na vilivyopungua fedha yake Sh. milioni 15 ipo tayari pamoja na fedha ya kumlipa fundi Sh. milioni 15 tunachokwama ni kibali ambacho hadi sasa hatujapatiwa," alisema Mumbi.

Mbambile Kisanjo, alisema kuwa wafadhili hao pia waliahidi kutembelea kitongoji hicho hivi karibuni kutoa msaada mwingine kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za madaktari.

Aidha, alisema kuna wananchi wanaishi maeneo ya vijijini hadi kufika barabara kuu ni kilomita zaidi ya saba na kwenda Kituo cha Afya Vigwaza inafika kilomita 21 jambo ambalo ni kikwazo kwa wazee, wanawake na watoto. Alisema zahanati inayojengwa Chamakweza ni kilomita 10 kwa wakazi wa Mbala bado ipo mbali na haijakidhi kupunguza umbali wa kufuata huduma za afya sababu hasa inayowafanya kuendelea kuomba kupatiwa kibali ili wananchi wanufaike na huduma karibu.

Pily Haji, mkazi wa Mbala Kijiweni, alisema gharama za kufuata huduma za afya mbali na kitongoji chao bado ni mzigo kwa wananchi pamoja na kuwapo kwa ujenzi wa zahanati Kijiji cha Chamakweza.

Ofisa Habari na Uhusiano wa Halmashauri ya Chalinze, John Mlyambate, alikiri kuwa na taarifa za maombi ya kibali cha ujenzi wa zahanati.

Hata hivyo, alisema kwa mujibu wa Sera ya Afya, kila kijiji kinatakiwa kuwa na zahanati moja na kata ni kituo cha afya kimoja hivyo tayari Kijiji cha Chamakweza ipo zahanati ambayo inajengwa.

Mlyambate alisema, wakazi hao awali walielezwa kuruhusu kutoa vifaa kwa ajili ya ujenzi wa zahanati ya Chamakweza, lakini hawakufanya hivyo na halmashauri inafuata sera za afya na ndio sababu ya kutotolewa kwa kibali.




Kamishna wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Aretas Lyimo, akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana kuhusu ukamataji wa dawa za kulevya uliofanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Kilimanjaro na Arusha pamoja maadhimisho ya Siku ya Kupinga Dawa za Kulevya yanayotarajiwa kufanyika jijini Arusha kuanzia Juni 23, mwaka huu. **PICHA: IMANI NATHANIE**

## YST yaomba serikali kuboresha mifumo ya elimu

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKISHO la Wanasayansi Chipukizi (YST), limeomba serikali kuboresha mifumo ya elimu itakayowezesha wanafunzi kushiriki katika mapinduzi ya viwanda.

Kauli hiyo ilitolewa na Mwanzilishi Mwenza wa YST, Dk. Gozibert Kamugisha, wakati akizungumzia maonyesho ya wanafunzi chipukizi ya sayansi ya kibunifu na kigunduzi yanayofanyika kila mwaka.

Dk. Kamugisha alisema dunia imeingia katika mapinduzi ya nne ya viwanda na kwamba Tanzania haipaswi kuwa mtazamaji bali mshiriki imara ikiwamo kuhakikisha miundombinu na mifumo ya elimu inaboreshwa kuwezesha wanafunzi kujiingiza katika eneo hilo.

Alisema ni muhimu Tanzania ikajiandaa na mapinduzi hayo yaliyojikita katika matumizi makubwa ya teknolojia.

"Kadri Tanzania inavyoelekea kwenye mapinduzi ya nne ya viwanda YST nayo imefanya juhudi za kuwandaa vijana wanaosoma shule za sekondari kuwa washiriki imara wa mapinduzi hayo kwa kuboresha ujuzi wa kisayansi na teknolojia kwa vijana," alisema Dk. Kamugusha.

Alisema kupitia mpango wa mafunzo shuleni, YST inawapatia vijana ujuzi wa kubaini matatizo ya kimaendeleo kwenye jamii zao na kubuni njia mbalimbali za kisayansi kukabiliana na matatizo hayo katika muktadha wa mapinduzi ya nne ya viwanda.

Kuhusu maonyesho ya wanasayansi Chipukizi, alisema wanafunzi hao watapata fursa ya kuonyesha kazi zao za kiteknolojia yanayotarajiwa kufanyika Desemba mwaka huu.

Alisema kazi za sayansi na teknolojia ambazo kwa sasa wanafunzi wanaendelea kuzitafiti zimejikita katika nyanja mbalimbali za sekta hizo na kwa mwaka huu maombi ya kazi za kisayansi 979 yalipokelewa na YST kutoka kwa wanafunzi wa shule za sekondari.

Alisema kazi hizo za kisayansi, zinajumuisha matumizi ya mifumo ya umwagiliaji kupunguza upotevu wa maji na kufanya mtawanyiko sawia wa virutubisho vya mimea katika udongo, virutubisho vya kibaiolojia kuzuia udumavu wa mimea na njia za kupunguza madhara ya mabadiliko ya tabianchi.

Alisema kazi nyingine zitakazoonyeshwa ni njia salama za usafirishaji maji na za kugundua upotevu wa maji kwa kutumia sensa.

Ofisa Mtendaji wa Taasisi ya Karimjee (KJF), Caren Rowland, alisema kazi za kisayansi zinazofanywa na wanasayansi chipukizi ni za kipekee ambazo zimekuwa chachu ya masomo ya sayansi shuleni.

Caren alisema YST imekuwa msaada mkubwa katika kukuza sayansi nchini kwa wanafunzi na kwa walimu pia.

# Zaidi kaya 700 kunufaika mpango biashara

**Na Stevie Chindiya,** TUNDURU

KAYA 726 za wanufaika wa Mfuko wa Kusaidia Kaya Maskini (TASAF) wilayani Tunduru, mkoani Ruvuma zimepangwa kunufaika na mradi wa mpango biashara zikiwa ni juhudi za serikali kuendelea kuwainia kiuchumi wananchi wake.

Mratibu wa TASAF Wilaya ya Tunduru, Muhidun Shaibu, alisema hayo wakati akiongea na wanufaika wa mradi huo wakati wa malipo.

Akifafanua alisema, kaya zilizoteuliwa kwa ajili ya majaribio zinatoka katika vijiji 11 kati ya 157 vilivyopo kwenye mradi huo.

Alisema endapo vitafanya vizuri kwa kuonesha manufaa, mradi huo utasambaa kwenye maeneo mengine ya mradi zikiwa ni juhudi za serikali kuwawezesha wananchi wake kiuchumi ili mradi ukifika mwisho wawe na uhakika wa vipato.

Alisema kupitia mradi huo wanufaika hao wamewezeshwa mitaji wa Sh. 350,000 kila mmoja baada ya kuibua shughuli za biashara ambazo wanaamini wakizifanya watapata mafanikio na kujikwamua kutoka katika umaskini uliopindukia.

Shaibu alisisitiza kuwa lengo la TASAF ni kuona mradi huo, unawawezesha walengwa kujitegemea na katika kipindi chote wanufaika hao pia wataendelea kunufaika kupitia mpango wa awali.

Aidha, katika taarifa hiyo Shaibu alivitaja baadhi ya vijiji hivyo kuwa ni Mtengashari, Matemanga Mchuruka, Mingu Mkandu, Mchekeni na Jiungeni.

Wakizungumzia mradi huo, baadhi ya wanufaika wa TASAF katika Kijiji cha Jiungeni, Kata ya Mchesi wilayani Tunduru, wameipongeza serikali kwa kubuni mradi.

Hamisi Mahamudu, aliibua mradi wa ufugaji mbuzi na kwamba ana imani kuwa mifugo hiyo itamsaidia kuinua uchumi wake baada ya kuzaliana na kuanza kuvuna.

Mnufaika mwingine, Mariamu Maganga alisema, alichagua mradi wa kufuga kuku na ana uhakika wa kupata mafanikio wakati wa kuanza kuvuna.

Wanufaika hao pia wameahidi kusimamia fedha walizopewa kwa ajili ya kutimiza mipango biashara waliyoiibua.

Mwezeshaji wa TASAF aliyesaidia shughuli za uibuaji wa miradi hiyo, Petro Komba, alisema baada ya malipo hayo wanufaika wanapewa wiki moja na watapita kufanya uhakiki kwa walengwa wote ili kujiridhisha kama wametekeleza malengo yao.

Alisema kwa wataozitumia fedha hizo tofauti na malengo hayo watatakiwa kuzirejesha na kuondolewa kwenye mradi.

## TANROADS yajitosa uhamasishaji usafi wa mazingira

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAKALA wa Barabara Nchini (TANROADS), umejitosa katika kuhamasisha usafi wa mazingira ili kuboresha afya ya jamii kwa wagonjwa wanaokwenda kufuata huduma za uchunguzi na tiba katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC.

Jana, Msimamizi wa Kitengo cha Fedha na Utawala wa TANROADS Mkoa wa Kilimanjaro, Deogratias Nachenga, alisema hatua hiyo inalenga pamoja na mambo mengine, kuhakikisha jamii inakuwa salama dhidi ya magojwa yanayotokana na uchafu wa mazingira.

TANROADS imetumia njia hiyo kuadhimisha wiki ya utumishi wa umma inayoongozwa na kauli mbiu 'uhusiano kati ya uwezeshaji wa vijana na usimamizi wa masuala ya uhamiaji; kujenga utamaduni wa utawala bora, matumizi ya TEHAMA na ubunifu katika utoaji wa huduma jumuishi.'

Alisema: "Wiki ya utumishi wa umma, imelenga kuwatumikia jamii na kurudisha upendo katika majukumu mengine yakiwamo ya usafi.

"Tumeamua kufanya usafi katika eneo ambalo wananchi wanapata huduma ili kudumisha mahusiano mazuri baina ya watumishi wa umma na wananchi."

Aidha, Ofisa Mazingira wa Hospitali ya Rufani ya KCMC, Jerome Mgeni, akizungumza na watumishi hao, alisema kitendo walichokifanya ni cha kiungwana na cha kupigiwa mfano kwa kurudisha upendo kwa jamii.

"Jamii ina dhana potofu ya juu ya watumishi wa umma, kwamba hawawezi kukuhudumia jamii bila malipo; jambo ambalo sio sahihi. Ni vyema watumishi wakashirikiana na jamii moja kwa moja," alisisitiza.

Hata hivyo, baadhi ya wakazi wa Longuo iliko hospitali hiyo, akiwamo Agness Mroso, alisema usafi wa mazingira, ni njia ya kuendeleza afya kwa kuzuia mawasiliano ya binadamu na athari za taka.

Alisema: "Usafi kama njia ya kuzuia maradhi, inaweza kutumika kwa usahihi kabisa ili kuzuia maradhi na milipuko ya magonjwa mbalimbali. Hivyo ni muhimu kufanya usafi katika mazingira yanayokuzunguka.

"Uboreshaji wa usafi wa mazingira una manufaa makubwa kwa afya ya wote katika kaya na katika jamii. Usafi wa mazingira unahusu pia udumishaji wa ratiba ya usafi, kwa njia ya huduma kama vile ukusanyaji wa taka na maji machafu."

# Waraibu wa dawa za kulevya Hospitali Bombo waongezeka

**Na Oscar Assenga,** TANGA

IDADI ya waraibu wa dawa za kulevya wanaopata huduma ya dawa za methadone katika Kituo cha MAT kilichoko Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga (Bombo), imeongezeka kutoka 173 hadi 896.

Kwa mujibu wa Kaimu Mkuu wa Kituo cha MAT, Dk. Joyce Diwi, takwimu hizo zimepaa katika kipindi kisichozidi miaka mitatu, kuanzia mwaka 2020 hadi Mei mwaka 2023.

Alikuwa akizungumzia jana maadhimisho ya huduma ya dawa za methadone na kampeni ya kupinga matumizi ya dawa za kulevya.

"Takwimu hizi zinatokana na usajili wa wagonjwa wanaopata huduma za MAT kutoka asasi za kiraia tatu, ambazo ni Gift of Hope, Tanga Drug Free na Organization Risk Behaviors.

"Hawa wamekuwa mstari wa mbele, kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya kwenye jamii," alisema.

Dk. Diwi, alisema kwa mwaka 2020 walisajili waraibu 173, ambapo wanaume walikuwa 162 na wanawake 11. Wakati mwaka 2021 walisajili waraibu 317.

Alisema mwaka 2022, walisajili waraibu 296 na kufanya jumla ya waraibu kufikia 786, ambapo wanaume walifikia 767 na wanawake 19. Kati ya Januari hadi Mei mwaka huu, wamesajili waraibu 107.

Awali akizungumza wakati wa maadhimisho hayo, Katibu Tawala Msaidizi, Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga, anayeshughulikia afya, Dk. Japhet Simeo, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kutoa fedha kuhakikisha huduma hiyo inapatikana kwenye hospitali hiyo.

Vilevile, Dk. Simeo, alisema wanamshukuru Rais Samia, kutokana na uwepo wa kituo hicho katika hospitali hiyo, ambacho kimekuwa msaada mkubwa kwa waraibu.

Mkurugenzi wa Kituo cha Sober House cha Gift of Hope kilichopo Kange jijini Tanga, Said Bandawe, aliishukuru Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga (Bombo), kwa huduma hiyo ambayo imekuwa ni msaada mkubwa kwa waraibu.



Washtakiwa wakiwa na mawakili wao baada ya kuachiwa huru katika shauri lao la ugaidi lililokuwa likiwakabili katika Mahakama Kuu Arusha. Aliyeshika joho mkononi ni Wakili Upendo Msuya aliyeongoza jopo la mawakili wa upande wa utetezi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Sheria inawalinda wanawake wanaotupa watoto'

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WAKILI mwandamizi wa serikali kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS) Mkoa wa Manyara, Rhoida Kisinga, amesema sheria inawalinda wanawake wanaotupa watoto wachanga ambao hawajatimiza mwaka mmoja kwa sababu ya kuhusishwa na matatizo ya afya ya akili.

Akizungumza na Nipashe jana katika mahojiano maalum, kuhusu wanawake wanaotupa watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja, alisema kosa la kutupa kichanga, linaangaliwa na ofisi hiyo kuanzia siku moja mpaka miezi 12.

"Kuua kichanga na kutupa kichanga hapo ni kesi mbili tofauti. Kwenye kutupa kichanga, tunaangalia siku moja mpaka miezi 12, lakini mtu akiua mtoto mchanga, anashtakiwa kama mtu aliyeua," alifafanua Wakili Kisinga.

Aidha, alisema ni kosa la jinai, kutupa mtoto ikipita miezi 12 na siku moja, kwa kuwa hayo yanahesabika ni mauaji, isipokuwa ndani ya miezi 12, mama akitupa mtoto inahesabika alikuwa na matatizo ya uzazi, ambayo yamemsukuma kufanya hivyo.


Alifafanua kuwa sababu kubwa wanayoitaja wanaokamatwa kwa kosa hilo, wengi wao hujitetea kwamba hawana kipato cha kutunza watoto waliowazaa, hivyo huishia kuwaza matunzo watayapata wapi.

"Sheria inamlinda mama huyu kuanzia siku moja mpaka miezi 12, ikiamini kuwa bado yuko kwenye matatizo ya uzazi," alisema Kisinga.

Akikazia hoja hiyo, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Babati, Victor Kimario, alisema sheria imeweka ukomo wa kipindi hicho cha miezi 12, kwa kuwa mama akitupa mtoto anakuwa amevurugika akili.

Kimario alisema katika kutoa hukumu juu ya kesi ya namna hiyo, huwa wanaangalia mazingira ya mama yalivyotokea.

Kuhusu afya ya kili, Dk. Yusuph Mwalunu kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, alisema mama anayefanya hivyo, mara nyingi chanzo chake ni wakati anapata ujauzito alikuwa na msongo wa mawazo, ambao unadumu mpaka baada ya kujifungua.





# Samia atimiza ahadi, awapa machinga kiwanja, mil.10/-

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SHIRIKISHO la Umoja wa Machinga wilayani Kahama mkoani Shinyanga limekabidhiwa kiwanja chenye hati miliki pamoja na Sh. milioni 10 zilizotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya ujenzi wa ofisi yao.

Katibu Mkuu wa shirikisho hilo, Venatus Magayane, aliyasema hayo jana wakati alipomtembelea Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita ofisini kwake.

Alisema kwa sasa wanaridhika na lengo la serikali katika kuhakikisha wanafanya kazi katika mazingira rafiki.

Alisema kila mkoa wenye wafanyabiashara hao, Rais Samia amewapatia Sh. milioni 10 na kiwanja chenye hati miliki kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za umoja wao.

Magayane alisema baada ya kukamilika kwa ofisi hizo machinga watakuwa na nafasi ya kukopesheka na taasisi za kifedha kulinganisha na ilivyokuwa awali kutokana na shughuli zao kuwa za kuhama.

Mwenyekiti wa shirikisho hiyo wilayani Kahama, Idrisa Kayombo, alisema kabla ya serikali kutoa maagizo ya machinga kutengewa maeneo, wao tayari walikuwa wameshapangiwa maeneo ya kufanya shughuli zao na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Anderson Msumba na kuwapatia mikopo isiyokuwa na riba.

Mmoja wa machinga, Agnes Magoli alisema ofisi hizo zitakapokamilika zitawasaidia kuwa wafanyabiashara wakubwa watakaokuwa wanachangia kodi serikalini.

Aidha, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Mboni Mhita, aliwaongezea Sh. milioni 1.5 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa ofisi yao, kuwataka viongozi kushirikiana pamoja na kutatua kero zinazowakabili ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa mitaji.




Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, akisoma ujumbe uliondaliwa na Shirikisho la Umoja wa Machinga wilayani hapo, walipomtembelea ofisini kwake kwa nia ya kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwapatia kiwanja na Sh. milioni 10 za ujenzi wa ofisi zao. **PICHA: SHABAN NJIA**

## RC awabana wakurugenzi h/shauri saba kuhusu mapato

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dk. Batilda Buriani, ameagiza wakurugenzi wa halmashauri saba mkoani Tabora kuhakikisha wanaongeza kasi ya ukusanyaji mapato katika maeneo yao.

Pia ameziagiza kuhakikisha zinavuka malengo kwa asilimia 100 au zaidi ifikapo Juni 29, 2023 lengo likiwa ni kufikia malengo ya mwaka wa fedha 2022/2023.

Alitoa agizo hilo juzi wakati akizungumza na madiwani pamoja na wakuu wa sekta na idara mbalimbali katika Halmashauri ya Wilaya ya Urambo.

Alisema Mkoa wa Tabora umejiwekea lengo la kukusanya Sh.bilioni 29 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 lakini hadi kufikia Juni 9, 2023 kiasi kilichokusanywa ni Sh.bilioni 26.6 sawa na asilimia 87.

Aidha, alisisitiza kuwa licha ya baadhi ya halmashauri kufanikiwa kufikia lengo la makusanyo, baadhi ya wakurugenzi kasi yao bado ni ndogo, hivyo akaagiza kila mmoja kuhakikisha anafikia asilimia 100 ya mapato kabla ya Juni 30, 2023.

Pia aliipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Uyui kwa kufanikiwa kuvuka lengo la mapato yao kabla ya Juni 9 kwani hadi sasa wamekusanya Sh.bilioni 3.5 sawa na asilimia 107 ya lengo la kukusanya Sh.bilioni 3.3.

Alitaja halmashauri nyingine zilizofanikisha makusanyo yao kwa asilimia 100 kuwa ni Manispaa ya Tabora waliokusanya Sh.bilioni 5.5, Kaliua Sh.bilioni 4.4 na halmashauri nyingine zikiendelea kupiga hatua zaidi.

# Wananchi wakumbushwa ulipaji ankara za maji

**Na Restuta Damian,** KAGERA

WANANCHI kutoka katika Wilaya ya Kyerwa na Bukoba mkoani Kagera wameshauriwa kushiriki katika uchangiaji wa ankara za maji kwa kufuata utaratibu uliowekwa, kuacha kufuata maneno ya wanasiasa.

Wito huo ulitolewa na Katibu wa Chombo cha Watumia Maji Ngazi ya Jamii (CBWSO), wilayani Kyerwa, Repius Diocres, wakati akizungumza na Nipashe juu ya tatizo la uelewa wa ulipaji ankara kwa watumiaji wa maji.

Alisema kila mwananchi ni mtumiaji wa maji hivyo suala la RUWASA wakimaliza kuweka miundombinu ni jukumu la wananchi kuitunza na kuigharamia.

Alisema lengo la kuundwa kwa chombo hicho ni kutaka jamii kuendelea kupata huduma na kuondoa tatizo la uhaba wa maji vijijini, hivyo ni jukumu la wananchi kuhakikisha miundombinu inakarabatiwa pale inapochakaa kupitia fedha wanazolipia maji.

Naye mtoa huduma wa ghati la maji Kijiji cha Lukindo Kata ya Katoma wilayani Bukoba, Fatma Abdu, alisema vyombo hivyo vimesaidia kuwapo na uimara wa miundombinua inayokuwa imeanza kutoa huduma.

Alitaja mgawanyo wa fedha inayolipwa na watumiaji hao kuwa ni Sh.50 kwa ndoo ya ujazo wa lita 20 na kati ya hiyo ni Sh.40 huingia katika mfuko wa uchangiaji maji na Sh.10 ni malipo ya msimamizi wa eneo hilo.

Meneja Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani Kyerwa, Mhandishi Shukrani Tungaraza alisema wakishajenga miradi hiyo kwa wananchi wanaunda vyombo hivyo kutoka katika jamii hiyo lengo likiwa ni kutunza miundombinu yake.

Alisema upatikanaji wa maji kwa wananchi ndani ya wilaya hiyo imefikia asilimia 61 na shughuli za ujenzi wa miradi kupitia makandarasi zinaendelea kufanywa na kuwataka wananchi kuwa sehemu ya miradi hiyo kwa kuchangia maji wanayotumia.

Naye Meneja wa RUWASA wilayani Bukoba, Mhandishi Evarsto Mugaya, alisema ili kukamilisha lengo la serikali la kumtua mama ndoo kichwani ni lazima wananchi wachangie ankara za maji.

## RITA yapewa kongole utoaji vyeti vya kuzaliwa

**Na Mwandishi Wetu,** SHINYANGA

WANANCHI mkoani Shinyanga wameupongeza Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) kwa kuendelea kusajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa ndani ya siku.

Pia wameipongeza RITA kwa kutoa elimu ya mirathi, kuandika na kuhifadhi wosia kwa wakazi wa mkoani Shinyanga ambao walijitokeza kwa wingi kupata huduma hiyo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na Nipashe wakazi hao wamesema kuwa RITA wamefanya kazi kubwa mbali ya kuwa na watu wengi waliokuenda kupatiwa huduma lakini wameweza kuwahudumia na kuwapatia vyeti vyao kwa siku moja.

Shija Kulwa mmoja wa wananchi hao alisema: “Nashukuru Mungu nimepata cheti changu, nilichangamkia fursa kama walivyotangaza na kweli nimekuja jana, leo cheti hiki hapa naondoka nacho, nawapongeza sana RITA wanapiga kazi hakuna usumbufu, hakuna nenda rudi”.

Mkazi mwingine wa Halmashauri ya Mjini Shinyanga, Seif Ayub alisema: “Kwa kweli mimi nimepatiwa huduma nzuri na sijaona ugumu wowote na nimepata cheti changu na uzee huu, hawa RITA wamenifumbua macho nilijua vyeti vya kuzaliwa ni watoto tu kumbe mpaka sisi vikongwe, nawashauri wazee wenzangu waje hii kitu ni muhimu sana”.

Akizungumza na waandishi wa habari, Ofisa Habari wa RITA, Goodluck Malekela, alisema kuwa wananchi kutoka maeneo mbalimbali wamejitokeza kwa wingi kusajiliwa na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa sambamba na elimu juu ya mirathi, kuandika na kuhifadhi wosia.

Aidha, aliwasihi wakazi wa Shinyanga na maeneo mengineo ambao bado hawajapata vyeti vya kuzaliwa wajitokeze ili wasipitwe na fursa hiyo.

“Wananchi wamejitokeza kwa wingi siku hadi siku, na sisi tupo vizuri tumejipanga tunawahudumia na vyeti wanaondoka navyo kama unavyoona, lakini pia elimu kuondoa dhana ya kwamba wosia ni uchuro, tunawaambia kwamba siyo kujichuria maana ukiandika utakufa na usipoandika utakufa,” alisema.

RITA imeweka kambi ya siku 10 mkoani Shinyanga kwenye viwanja vya Sabasaba Manispaa ya Shinyanga kuanzia Juni 11 hadi 20, mwaka huu ikiendelea kutoa huduma ya usajili vyeti vya kuzaliwa na kutoa elimu juu ya mirathi, kuandika na kuhifadhi wosia.



Ukurasa 12

Waliokatiza masomo waambiwa kila kitu kipo, wachangamkie shule




Ukurasa 14

Nishati safi jikoni kwa kila Mtanzania inawezekana, Umoja wa Ulaya wajitosa

Nipashe
# TESA
Jumanne Juni 20, 2023
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI




Ukurasa 13

**Singapore yawa taifa pekee kunapoliwa kitoweo cha kutengenezwa maabara**

TEKNOLOJIA
NA PILLY
KIGOME

ROSETTLE LOWHIM

# Injinia aliyeshinda usaili lakini akatoswa ajira, kisa mwanamke

• Ni mgunduzi mahiri akihusika na jiko sanifu

ROSETTLE Lowhim ni mwanafunzi wa shahada ya uzamivu ya uhandisi katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam [DIT], ambaye amekuwa pambo na chachu kwa wengine kwa namna anavyojitahidi kuitumia teknolojia kubadilisha maisha yake na ya wengine.

Akiwa bado masomoni ameunda mashine kadhaa zinazotumiwa na mafundi vyuma anaposema mwaka 2021 hadi 2022 akiwa mwaka wa tatu wa shahada ya kwanza ya Uhandisi Mitambo (mechanical engineering) alibuni na kutengeneza mashine za urembo unaotokana na kukunja vyuma.

Anaitambulisha kama 'semi automatic metal scrolling and twisting machine' inayotumiwa kukunja vyuma kutengeneza urembo kwenye madirisha ya grili, milango, mageti na mapambo mbalimbali.

Mara nyingi urembo wa madirisha, vitanda, milango, meza, uzio na mapambo mengine hutengenezwa kwa kukunja na kusuka nondo au 'square pipes na flat bars na pengine hakukuwa na mashine ya kuzikunja kupata maumbo mbalimbali bali kazi hizo hufanyika kienyeji.

Rosettle anasema mbali na mashine hiyo pia amegundua na kutengeneza nyingine ya kubangua karanga [groundnut cracking machine] ambayo tayari iko sokoni.

Kadhalika anasema amebuni jiko maalum la umeme la kukaangia crips na chips linalotumia nishati kidogo lakini likifanyakazi kwa ufanisi mkubwa na kusaidia kupunguza matumizi ya mkaa na kuni yanayochangia kuharibu misitu na kuchochea mabadiliko ya tabianchi.

### ANATAJA PAGUMU

Msomi anakumbushia kuwa licha ya juhudi na jitihada za kufanikisha maendeleo ya sayansi na teknolojia, anakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na kutoaminika kwenye ajira kwa vile ni mwanamke, hivyo kukosa kazi.

Anasema kutokana na jinsi yake mbali na kuwa na uwezo mkubwa kufanya vizuri katika kazi lakini inamuwia vigumu kuaminika kikazi jambo linalomshangaza na kumuumiza msomi huyo.

Anaendelea kuiambia Nipashe kuwa, amewahi kukosa kazi kutokana na jinsi yake (KE) katika moja ya kampuni kubwa nchini (jina tunalihifadhi) alipokwenda kufanya usaili.

Anasema aliambiwa kuwa amefaulu kwenye usaili lakini baadaye mkuu wa kampuni alipogundua ni mwanamke, akamkataa akakosa kazi hiyo, japokuwa alifanya vizuri katika usaili na kuibuka kidedea.

Rosettle anafafanua kuwa ndoto zake kubwa ni kuja kumiliki karakana ama kampuni kubwa ya kisasa nchini itakayoweza kuhudumu ndani na nje ya mipaka kwenye masuala ya teknolojia na uhandisi.



Mhandisi Rosettle Lowhim wa DIT akiwa kazini kutengeneza mashine ya kubangulia karanga. **PICHA: MWANDISHI WETU**

### KUCHOCHEA WANAWAKE

Ubunifu na mabadiliko ya teknolojia ni chachu ya kuleta usawa wa kijinsia, ni kauli mbiu ya kitaifa inayotumiwa kuwachochea wanawake kama sio kuwatoa kimasomaso mijini na vijijini katika kujihusisha na kunufaika na teknolojia.

Lengo ni ili usawa unapatikane kupitia nyanja hiyo, na kuwaamsha wanawake wengi ambao wamebaki nyuma na kukosekana usawa kiteknoloji na hata kijinsia.

Mtandao wa Jinsia Tanzania [TGNP] na Chuo cha DIT, wanaingia ubia kusaidia kufanikisha kazi za ubunifu za kiteknolojia na kutatua changamoto za kijinsia kama sehemu ya kuwapa fursa na hamasa wasichana wanafunzi kufanya vizuri katika eneo hilo 76la sayansi na teknolojia.

Taasisi hizi zimetengeneza kanzi data inayoitwa Tanzania Women Connect Portal inayohifadhi kazi za wanawake katika nyanja mbalimbali itakayowezesha kupata na kunufaika na fursa mbalimbali kwenye harakati za kuleta usawa wa kijinsia nchini.

Mwenyekiti wa Bodi TGNP, Gemma Akilimali, anaiambia Nipashe kuwa kuwawezesha wanawake na makundi mengine katika teknolojia kuna matokeo chanya hasa katika ubunifu ili kupata suluhisho kwa shida za kijamii na uvumbuzi mwingine unaowasaidia wanawake na watoto wa kike kupata mahitaji ili kuchochea ufikiwaji wa usawa wa kijinsia.

ELIMU
NA CLAUDIA KAYOMBO

# Waliokatiza masomo waambiwa kila kitu kipo, wachangamkie shule

KUNA msemo ukimwelimisha mtoto wa kike umelifundisha taifa au jamii nzima. Hili linamaanisha kuwa mwanamke ndiye anabeba majukumu mazito ya kulea familia hivyo, anapokuwa amejengeka kitaaluma, stadi na mafunzo ya aina mbalimbali taifa haliwezi kutetereka.

Serikali ya awamu ya sita kwa kutambua hilo imeanza kutekeleza mradi wa kuimarisha ubora wa elimu ya sekondari kwa njia mbadala (SEQUIP) ukilenga mabinti ambao wameshindwa kusoma kwa sababu mbalimbali.

Lengo serikali inasema ni kumpa fursa ya kupata elimu mtoto wa kike aliyepatwa na madhila ikiwamo mimba za utotoni, maradhi au, shida za wazazi na matatizo ya kifamilia na kushindwa kumaliza kidato cha nne.

Mradi huo unalenga kuwafikia wasichana 12,000 nchi nzima wenye umri wa kati ya miaka 13 hadi 21 katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka jana, anasema Mratibu Msaidizi wa SEQUIP, kutoka Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW), Amina Abubakari.

Ni wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wawezeshaji wa somo la stadi za maisha kutoka vituo vinavyotoa elimu mbadala kupitia mradi huo, Mratibu wa SEQUIP Amina anaeleza kuwa wasichana walioacha masomo kutokana na sababu mbalimbali waende vituoni kwani wanapatiwa elimu bure na serikali.

Anafafanua kuwa katika kufanikisha lengo hilo serikali imeandaa moduli za kufundishia zinazompa urahisi wa kujifunza kwa muda wa miaka miwili mlengwa.

Amina anasema licha ya somo hilo la stadi za maisha, pia kemia na fizikia ambayo awali hayakuwamo sasa yameingizwa katika mfumo huo ambao mwanafunzi anasoma bure wakati serikali ikimlipia hadi ada ya mitihani ya taifa.

Wakati wa mafunzo hayo yanayowakutanisha pamoja wawezeshaji wa somo la stadi za maisha takriban 85 kutoka mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Tabora, Arusha, Manyara, Simiyu, Shinyanga, Dodoma, Mara, Kigoma na Singida, mratibu huyo anabainisha kuwa lengo ni kujengewa uwezo wa kutumia njia shirikishi za ufundishaji zinazozingatia ujengaji wa umahiri kwa wanafunzi.



Mwenyekiti wa Baraza la Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Dk. Naomi Katunzi, inayofanikisha mafunzo SEQUIP. **PICHA: MTANDAO**

> "Mwongozo wa masomo yao ni mzuri unamwezesha wakati mwingine hata kujisomea mwenyewe nyumbani lakini hili la kukaa karibu na eneo wanalofundishwa ni jambo jema.

"TEWW tulijiwekea lengo la kuwafikia wasichana 3,000 kila mwaka kuendelea na masomo ya sekondari, ninayo furaha tuliweza kusajili walengwa 3,333 mwaka uliopita wa 2022 na huu 2023 tumesajili wasichana 3,616 sawa na asilimia 120.5," anasema Amina.

Anabainisha kuwa mradi huo ulioanza mwaka jana utafikia tamati mwaka 2026 na kwamba katika kipindi cha mwaka jana wasichana 3,333 walisajiliwa katika vituo 131 nchini huku mkoa wa Mbeya ukiongoza kwa kusajili wasichana 472 ukifuatiwa na Mwanza.

"Tangu kuanza kwa mradi huu unaosimamiwa na Wizara ya Elimu na TAMISEMI kwa kushirikiana na Benki ya Dunia (WB) tumeanza kwa mafanikio makubwa ambapo vituo kwa ajili ya mradi huo vimeandaliwa moduli za kujifunza kumwezesha msichana kujifunza kwa urahisi hata akiwa nyumbani. Baada ya kuhitimu na iwapo watafaulu vizuri watachaguliwa kujiunga na vyuo vya kati kote nchini."

Mkuu wa Wilaya ya Singida, Pasikasi Muragili, akifungua mafunzo anaipongeza menejimenti ya TEWW na mikakati iliyoleta mradi wa SEQUIP kwa kuandaa na kuendesha mafunzo hayo muhimu katika kutekeleza mradi huo.

Muragili anasema huo ni mwendelezo wa nia njema ya serikali ya awamu ya sita ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, wa kutoa elimu bila malipo na sehemu ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kitaifa na kimataifa.

"Tunampongeza Rais kwa dhamira yake njema ya kumkomboa mtoto wa kike, washiriki zingatieni yale yote yatakayoelekezwa ili kuongeza ufanisi katika ufundishaji wa stadi za maisha kwa wasichana wanaoendelea na masomo katika vituo mbalimbali ambao ndoto zao zilikatishwa," anasema.

Mkuu wa Wilaya anaongeza kuwa kinachofanywa na serikali ya awamu ya sita ni kusimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM inayoelekeza kuongeza fursa ya upatikanaji elimu kwa makundi mbalimbali wakiwamo wasichana hao.

Anaagiza licha ya kuwafundisha pia wafuatilie nyendo zao baada ya elimu ili kubainisha matokeo mazuri ya wasichana hao kupitia jitihada za Rais Samia kuwarudisha shuleni.

Mmoja wa washiriki Mwalimu Catherine Luwa, kutoka mkoa wa Singida, akizungumza baada ya ufunguzi anamshukuru Rais Samia kwa kufanya jambo hilo kubwa la kuwarudisha shule wasichana waliokatisha masomo ya sekondari kutokana na sababu mbalimbali.

Anaeleza kuwa mafunzo hayo yana mwelekeo wa kuwajengea uwezo zaidi wa namna ya kuwafundisha wasichana hao ambao bila shaka miongoni mwao siku zijazo watakuja kushika nyadhifa mbalimbali serikalini.

Mkufunzi mkazi kutoka Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima mkoani hapa, Abtwalibu Salimu, anasema kupitia mradi huo mkoa wa Singida katika kipindi cha mwaka jana ulisajili wasichana 114 waliokubali kurejea shule ambao wanasoma katika vituo vya Iramba, Singida Manispaa na Mkalama.

Ofisa Elimu ya Watu Wazima na Eimu ya Nje ya Mfumo Rasmi, wilayani Manyoni, Emmanuel Mwarabu, anasema moja ya changamoto wanayokutana nayo wasichana hao ni umbali kutoka maeneo wanayoishi na vituo vya kujifunzia vilipo.

Anatoa wito kwa serikali kwamba dhamira njema ya kuwarudisha shule wasichana hao itafikia malengo iwapo watajengewa mabweni akisema: "Kuna wengine wanaweza kuvunjika moyo kutokana na umbali kutoka wanakoishi hadi vituo vyao vya kusomea vilipo.

"Mwongozo wa masomo yao ni mzuri unamwezesha wakati mwingine hata kujisomea mwenyewe nyumbani lakini hili la kukaa karibu na eneo wanalofundishwa ni jambo jema," anasema Mwarabu.

### WAHUSIKA WAMULIKWE

Mwalimu Sospeter Makwaia kutoka Sengerema mkoani Mwanza, anakazia kuwa kuna haja kwa serikali kuweka mazingira ya kusomea wasichana hao ili lengo la kuwarudisha shule liweze kutimia miongoni mwa wengi wao.

Anasema uzoefu unaonyesha wachache miongoni mwa wasichana hao wavulana waliowasababishi ujauzito bado wanaendelea kuwa na uhusiano nao wa kimapenzi hadi sasa hali ambayo kutokana na umri wao inaweza isifanikishe lengo lao kurudi shuleni kwa mara ya pili.

Mwalimu Makwaia pia anashauri hamasa zaidi ya kuwarudisha shule wasichana hao kwani anaamini wengi wa walio majumbani watahusika kurudi shule.

SAYANSI
NA MWANDISHI WETU

NYAMA MBADALA

# Singapore yawa taifa pekee kunapoliwa kitoweo cha kutengenezwa maabara

ONGEZEKO la hewa ukaa duniani au gesi chafu linachangiwa na kufuga wanyama wengi kienyeji kama inavyofanyika kwenye mikoa ya Kanda ya Ziwa, Manyara na Arusha.

Wafugaji wa ng'ombe na wanyama wengine wanaocheua kama mbuzi na kondoo, wanaarifiwa kuwa mifugo hiyo hutoa 'methane', gesi chafu inayoongeza joto angani pale wanapoyeyusha nyasi na mimea.

Mchakato huo huitwa 'enteric fermentation' au "uchachushaji wa ndani ya tumbo," ndiyo asili ya kucheua kwa wanyama hao. Gesi ya methane pia hutolewa kutoka kwenye samadi na mkojo wa mifugo vyote huongeza joto duniani.

Ili kukabiliana na hali hiyo wanasayansi wameanza kuzalisha nyama kwenye maabara wakizilisha na kuzikuza seli za vipande vidogo vya minofu.

Ndicho kinachoendelea nchini Singapore na wateja huila migahawani bila kikwazo ikisifiwa na kila ailaye, kwa mfano: "Inaonekana kama kuku, ina harufu na ladha ya nyama ya kuku. Huwezi kuhisi kama kipande cha nyama kilicho mbele yako hakikutoka bandani. Kumbe imetengenezwa katika maabara viwandani..." inaandika BBC Swahili.

Ni ndani ya mgahawa wa Huber's Butchery and Bistro nchini Singapore, ambao ndiyo pekee duniani unaouza nyama ya kutengenezwa na maabara katika menu yao. Kitalaamu huitwa minofu inayotengenezwa kutokana na seli za wanyama.

Wateja wanaotumia nyama hiyo wana maoni kwa mujibu wa mmiliki wa maelezo ya mmiliki wa mgahawa, anayeongea na BBC, akiwanukuu wakisema ni nyama ya kimaadili, ni safi na bila kuathiri au kupunguza ladha.

Mabilioni ya dola yanamiminwa kwenye tasnia hiyo, tangu mkate wa nyama au burger ya kwanza ya kitoweo kilichokuzwa katika maabara ambao uligharimu Dola $330,000 au pauni £263,400.

Tangu mkate huo ulipozinduliwa London mwaka 2013, kampuni kadhaa duniani zimejiunga na harakati za kuleta nyama ya bei nafuu sokoni.

Kufikia sasa, ni kampuni ya 'Eat Just' pekee ambayo imeidhinisha bidhaa yake kuuzwa kwa umma baada ya wasimamizi nchini Singapore ambayo ni taifa pekee duniani kuruhusu nyama iliyokuuzwa kwenye maabara kuuzwa, biashara iliyoanza Desemba 2020.




Ni nyama inayotengenezwa maabara. **PICHA: FOOD FOR THOUGHT**

Baada ya miezi michache mwaka huu Huber's imeanza kutoa sandwich au mikate iliyowekewa kuku na sahani ya tambi au pasta ya kuku kwa wateja ingawa ni mara moja pekee kwa wiki na sehemu ndogo za kulia zinapatikana si kila mahali.

"Nyama ya kuku ya kukuzwa kwenye maabara ni nyama halisi hivyo siyo lazima kuchinja mnyama," anasema Josh Tetrick, Ofisa Mkuu Mtendaji wa kampuni ya "Eat Just", akizungumza na BBC kutoka San Francisco. "Njia hii ya kupata kitoweo ina maana na umuhimu kwa siku zijazo," anasema.

Tofauti na ile inayotengenezwa na mimea, nyama inayouzwa kwenye maabara ni halisi, mchakato wake unahusisha kutoa seli kutoka kwa mnyama, ambazo hulishwa na virutubisho kama vile protini, sukari na mafuta na hatua kwa hatua huwa minofu.

Seli hizo zinaruhusiwa kugawanyika na kukua, kabla ya kuwekwa kwenye chembechembe kubwa ya kibaiolojia ya chuma, ambayo hufanya kama tangi na kuchachusha na kwamba baada ya wiki nne hadi sita, 'huvunwa' kutoka kwenye kinu cha kibaolojia.

Protini fulani ya mboga huongezwa, kisha hutengenezwa, kupikwa na kuchapishwa kwa kutumia teknolojia ya 3-D ili kuipa sura na ulaini unaohitajika kama wa nyama halisi ya kuku.

"Ni nyama, ni kamilifu!" Anasema Caterina, mteja aliyefika mgahawani hapo ili kujaribu kuku wa kukuzwa kwenye maabara".

Sahani ya tambi ya kuku huuzwa Dola za Singapore $18.50 au Dola za Marekani $13.70; takribani pauni £11, lakini hiyo imepunguzwa sana ikilinganishwa na gharama ya sasa ya kuzalisha nyama hiyo.

Eat Just haitasema ni kiasi gani hasa inachotumia kutengeneza kuku wake wa kukuzwa kwenye maabara, lakini uzalishaji wa kampuni hiyo unatoa kilo mbili au paundi 4.4lb au kilo 3.0 kwa wiki nchini Singapore.

> Ni nyama, ni kamilifu!" Anasema Caterina, mteja aliyefika mgahawani hapo ili kujaribu kuku wa kukuzwa kwenye maabara.

BBC inasema kwa kulinganisha uzalishaji huo na kilo 4,000 hadi 5,000 za kuku wa kawaida inayouzwa kila wiki huko Huber pekee , inakupa picha ya ukubwa wa kazi iliyo mbele, kwa ufupi, watahitaji kuongeza uzalishaji kwa kiasi kikubwa ili kuepuka kupata hasara kwa kila kipande cha kuku.

### NI WASIWASI TU

Kinadharia, kupunguza utegemezi wa dunia wa ardhi na mifugo kwa ajili ya kuzalisha nyama kunafaa kupunguza utoaji wa kaboni, lakini kwa sasa teknolojia ya hali ya juu inayohitajika kuunda nyama ya kukuuzwa ni ghali mno kiasi kwamba inatumia faida yote.

Utafiti wa Chuo Kikuu cha California, ulikadiria kuwa mchakato huo hutoa kati ya mara 4 na 25 zaidi ya kaboni dioksidi kuliko nyama ya kawaida ya ng'ombe. Hata hivyo, East Just imeuita utafiti huo kuwa una dosari".

Anapoulizwa na BBC kama mradi mzima unaweza kuishia bila mafanikio, Josh Tetrick kutoka Eat Just akiijibu: "kwa hakika".Lakini bado hajakata tamaa kutengeneza nyama kwa njia hiyo anayosema ni muhimu."

"Sio moja kwa moja. Ni vigumu. Haina dhamana na inaweza isifanyike. Lakini chaguo lingine kwetu ni kutofanya chochote. Kwa hivyo tuliamua kuchukua dau na kuichukua hatua hii."

Wawekezaji wengi wameamua kufanya dau kama hilo. Kufikia mwaka huu, inakadiriwa Dola za Marekani bilioni 2.8 zimetumika katika kuendeleza nyama ya maabara.

Hata hivyo, ikiwa nyama iliyokuuzwa kwenye maabara itakuwa ni mbadala kwa watu walio na uwezo mkubwa katika dunia au nchi zilizoendelea, basi kutegemea uwekezaji huo kufanywa na watu binafsi kunaweza kukwama.

Serikali, zitahitaji kuweka fedha nyingi katika nyama ya kukuuzwa kwa njia hii ili kushindana na kitoweo cha mifugo iliyochinjwa baada ya kutunzwa na kulishwa kwenye mashamba ya wakulima."Hii ni kama mpito au kama ilivyo kwenye kusaka nishati mbadala. Kuna kazi ngumu zaidi."

TEKNOLOJIA
NA RESTUTA JAMES

# Nishati safi jikoni kwa kila Mtanzania inawezekana, Umoja wa Ulaya wajitosa

• Kitakachotumika kupikia gesi, bioethanol, mkaa wa mimea




Baadhi ya washiriki wa uzinduzi wa kampeni ya Anzia Jikoni, pamoja na mtaalamu wa masuala ya fedha wa UNCDF, Imanuel Muro (kulia). **PICHA: RESTUTA JAMES**

MOJA kati ya malengo endelevu ya dunia (SDGs) ni kuona kuwa ifikapo 2033, karibu kaya zote zitumie nishati safi na salama kupikia.

Malengo yanataka itakapofika mwaka huo, asilimia 80 ya kaya zote jiko lake liwe linatumia maijiko banifu ya kuni au mkaa kupika kwa ufanisi au kimiminika kinachowaka cha bioethanol kinachozalishwa kutokana na mimea yenye sukari nyingi ikiwamo miwa.

Majiko mengine yanayolengwa ni yale yanayotumia gesi ya kwenye mitungi LPG na hata umeme lakini kiasi kidogo, tena yakiivisha vyakula kwa ufanisi.

Ni kazi inayofanikishwa na mageuzi ya kiteknolojia ya uvumbuzi wa majiko yanayotumia nishati kidogo kupikia na kuhakikisha upatikanaji wake kwa wananchi ni wa gharama nafuu ili watu wa hali zote mijini na vijijini wamudu.

Katika kufikia azma hiyo Ofisi ya Umoja wa Ulaya (EU), nchini imetenga Euro milioni 17, takribani Shilingi bilioni 47.6, kuzisaidia kampuni zinazojishughulisha na uzalishaji na usambazaji wa nishati pamoja na majiko hayo ya kisasa, ili kufikia azma ya dunia ya kukabili athari za mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira, unaotokana na nishati chafu.

Mtaalamu wa masuala ya Fedha wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mitaji ya Maendeleo (UNCDF), linalosimamia utekelezaji wa Mradi wa Cookfund, Imanuel Muro, anasema mageuzi ya kiteknolojia ni muhimu ili kupunguza matumizi ya nishati zote za kupikia.

Anasema kupunguza matumizi kutawezekana kwa kuruhusu uvumbuzi wa majiko yanayotumia kiasi kidogo cha nishati, bila kuathiri upishi ili kaya nyingi zione umuhimu wa kutumia teknolojia mpya.

Muro ambaye ni meneja mradi wa Cookfund, anasema mageuzi ya kiteknolojia yaliyoleta majiko banifu ya mkaa na kuni, ya gesi yanayotumia gesi kidogo, bioethanol na ya umeme yanayotumia umeme kidogo, yameshafanyika.

Anasema katika hilo, kuna mkaa na kuni rafiki wa mazingira (green charcoal), ambao unatokana na mimea ikiwamo miti inayoweza kukuzwa kwa kipindi kifupi, ambao ukipatikana kwa wingi utapunguza ukataji wa miti ya asili kutengeneza mkaa na kuni.

> Linatumia nishati kidogo kuivisha chakula kwa muda mfupi na kuhifadhi virutubisho hivyo kuokoa muda, fedha, afya na mazingira; unaweza kuivisha maharage kwa umeme wa Sh. 200.

Anasema uvumbuzi mwingine umeleta majiko yanayotumia kuni na mkaa kidogo: "Unaweza kuona kwamba pamoja na kuwa na mkaa rafiki wa mazingira, teknolojia imetuletea majiko yanayotumia nishati hii kwa kiasi kidogo sana. Majiko haya yanapunguza matumizi ya mkaa kwa asilimia 60 na yamethibitishwa," anasema Muro.

Aidha, anataja jiko linalotumia gesi kidogo, umeme, bioethanol na gesi kidogo ambayo yakipatikana kwa wingi yatafanikisha kukabili athari za uharibifu wa misitu kwa kukata kuni na mkaa.

"Tunachopaswa kufanya ni kubadilisha mitazamo yetu na kutumia nishati hizi rafiki, ili tuweze kuokoa mazingira yetu na hili ndilo suluhisho," anasema.

Ili kuweza kubadili mtazamo, UNCDF imezindua kampeni ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ya 'Anzia Jikoni-mabadiliko ya hewa safi ya baadaye yanaanzia jikoni.'

Anasema kupitia kampeni hiyo, mradi wa Cookfund unalenga kufadhili kampuni na wajasiriamali wanaojihusisha na uzalishaji na usambazaji wa nishati safi.

"Huwezi kupunguza ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa bila kuleta mabadiliko ya nishati ya kupikia. Ufadhili wa EU unalenga ubunifu wa teknolojia ya kisasa ya kupata majiko yanayotumia mkaa, gesi na kuni kidogo. Tunatoa ruzuku kwa kampuni ili mtumiaji wa mwisho aweze kupata nishati na jiko kwa bei ndogo," anasema.

Muro anasema kampeni ya 'Anzia Jikoni' inalenga kuueleza umma umuhimu wa matumizi ya teknolojia za kupikia zinazopunguza madhara ya athari za mabadiliko ya tabianchi.

Anatoa mfano kwamba kwa kaya zinazotumia kuni kwa ajili ya kupikia, mageuzi ya teknolojia yanaziwezesha kuendelea kutumia nishati hiyo kwa kiasi kidogo, wakiwa na jiko sanifu badala ya kutumia mafiga yanayohitaji kuni nyingi na kupoteza pia moto.

"Huwezi kumwambia mtu ambaye yuko kijijini anayepata kuni za bure atumie umeme au anunue gesi akakuelewa. Jiko sanifu linaweza kumshawishi kwa sababu linamsaidia kupunguza matumizi ya kuni na wakati huo huo, chakula chake kinaiva kwa wakati," anasema.

Muro anaongeza: "Ufadhili wa EU unalenga kuongeza utaalamu wa kifedha katika uwekezaji ili kuchochea uwezo wa kampuni katika kuvumbua teknolojia safi za kupikia."

Anasema mradi unalenga kuongeza matumizi ya teknolojia za kisasa za kupikia kwa kuhakikisha upatikanaji wake kwa urahisi.

Maelezo ya Muro yanaungwa mkono na Mratibu wa Kitaifa wa Mradi ya Nishati na Mazingira wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO), Victor Akim, ambaye anasema matumizi ya nishati yanaendelea sambamba na majiko yanayotumia nishati kidogo.

"Tunahimiza matumizi ya majiko yanayopunguza matumizi ya nishati ili kila kaya ipate unafuu. Hili litasaidia kukabili athari za kimazingira," anasema.

Anasema UNIDO inafadhili viwanda vinavyozalisha majiko na nishati mbadala ya kupikia, ili kuwezesha upatikanaji wake kwa wingi.

Ofisa Ufuatiliaji na Tathmini wa Cookfund, Elizabeth Ngoye, anasema ndani ya miezi mitatu, watumiaji wapya 3,373 wamefikiwa na nishati safi ya kupikia, katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma na Mwanza, inayohusika kwenye mradi huo.

Kadhalika anasema mradi unalenga kuzifikia kaya mpya 580,000 na kuzalisha ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja, kupitia kampuni 295 zinazokusudiwa kufadhiliwa kifedha na kiufundi.

Mvumbuzi wa jiko linalotumia umeme kidogo, Shukuru Meena, anasema jiko hilo sanifu linapika kwa kutumia presha ya mvuke unaokusanywa ndani ya sufuria.

"Linatumia nishati kidogo kuivisha chakula kwa muda mfupi na kuhifadhi virutubisho hivyo kuokoa muda, fedha, afya na mazingira; unaweza kuivisha maharage kwa umeme wa Sh. 200," anasema Meena.

Anasema jiko hilo ambalo linamuundo kama lile la kupikia wali, linauwezo wa kupika vyakula vya aina mbalimbali kama maharage, ndizi, kande, mchemsho, ugali na pilau kwa njia ya kuchemsha, kurosti, kukaanga, kupika kwa mvuke na kuoka.



## Waziri wa Afya akiri tatizo ukosefu wa dawa bado lipo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amekiri kuwa pamoja na jitihada za serikali kuongeza bajeti ya dawa hadi kufikia Sh. bilioni 200 bado kuna malalamiko mengi ya wananchi kukosa dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

Aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye kilele cha wiki ya famasi, kueleza kuwa pamoja na jitihada za serikali kuongeza bajeti ya dawa na vifaa tiba lakini bado yapo malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kukosa dawa katika vituo vya afya.

"Kama mnavyofahamu Rais Samia Suluhu Hassan ameongeza bajeti ya dawa hadi kufikia Sh. bilioni 200 na hadi sasa tumeshapokea Sh. bilioni 184 ambayo ni asilimia 94 ya bajeti nzima na inawezekana hadi Juni 30 tutakuwa tumepata kwa asilimia 100 ya bajeti yote," alisema.

Alisema Rais ametimiza wajibu wake wa kutoa fedha hivyo kamati za dawa na vifaa tiba lazima zikae na kujadili ili kubaini nini tatizo la vituo vya afya kukosa dawa.

Aidha, alisema kero kubwa kwa wananchi katika sekta ya afya ni kukosekana kwa vipimo wanapovihitaji pamoja na kuandikiwa dawa lakini hawazipati katika vituo vya afya.

Kadhalika, aliwataka wafamasia nchini kutekeleza majukumu yao ya kila siku kwa kuzingatia weledi na miongozo ya utoaji dawa.

Naye Msajili wa Baraza la Famasi nchini, Elizabeth Shekhalage, alisema lengo la maadhimisho ya wiki hiyo ni pamoja kujitathmini katika utendaji wao wa kazi wa kila siku.

# Askari mstaafu amwomba Samia kupata malipo fidia ya mil.200/-

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MWANAJESHI Mstaafu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Mughenyi Selemani (84) amemwomba Rais Samia Suluhu Hassan amsaidie kupata malipo ya fidia ya ardhi ya Sh.milioni 200 anayolidai Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO).

Akizungumza jana na waandishi wa habari Mjini Singida, Mughenyi alisema kwa zaidi ya miaka 30 amekuwa akifuatilia madai hayo SIDO ambao walichukua eneo lake lenye ukubwa wa ekari 20 lililopo katika Kata ya Utemini Manispaa ya Singida tangu mwaka 1971 na kujenga makao makuu ya ofisi za shirika hilo Mkoa wa Singida.

Alisema amekuwa akifuatilia madai hayo na kuandika barua katika ofisi mbalimbali za serikali ikiwamo ofisi ya Waziri Mkuu, Waziri wa Viwanda na Biashara, Mkuu wa Mkoa wa Singida na Mkuu wa Wilaya ya Singida lakini bado hajapata stahiki zake.

"Juni 2016 ofisi ya SIDO makao makuu waliandika barua na kuniahidi kuwa wangeweza kunilipa madai yangu lakini tangu kipindi hicho hadi sasa wamekaa kimya na kila anapoandika barua nyingine kukumbushia zimekuwa hazijibiwi na viongozi wa SIDO," alisema.

Alisema tangu aandikiwe barua hiyo ni miaka saba sasa SIDO wamekuwa kimya hakuna kinachoendelea na kila akiwaandikia barua kukumbushia hazijibiwi. "Nimeitumikia serikali yangu kwa uaminifu na uadilifu mkubwa katika nafasi mbalimbali za uongozi hadi nikastaafu lakini leo hii suala langu linashindwa kufanyiwa kazi, bado nina imani kubwa na serikali yangu litafanyiwa kazi najua suala hili kuna watu wachache wanataka kunidhulumu haki yangu," alisema.

Alipotafutwa na Nipashe kuhusu madai hayo, Mkurugenzi Mkuu wa SIDO, Sylivester Mpanduji, alikiri kufahamu madai ya mwanajeshi huyo na kusema kwamba kwa sasa suala hilo lipo Ofisi ya Rais.




Mkurugenzi Mshiriki wa kampuni ya ukaguzi wa hesabu ya EY anayeshughulikia Huduma za Ushauri wa Kodi, Beatrice Melkiory, akizungumza katika mjadala wa bajeti ulioandaliwa na kampuni na kuwashirikisha wataalamu kadhaa wa masuala ya uchumi na fedha uliofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TEC yapendekeza kutumika mfumo wa uchumi soko jamii

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BARAZA la Maaskofu wa Katoliki Tanzania (TEC), limetupia jicho mfumo ambao unaongoza shughuli za kiuchumi za Watanzania na kuhamasisha kutumika kwa mfumo wa uchumi soko jamii unatumiwa na nchi mbalimbali ikiwamo Ujerumani ili kupata mafanikio zaidi.

Katibu Mkuu wa TEC, Padri Dk. Charles Kitima, aliyasema hayo jana jijini hapa katika mjadala kuhusu fursa za kiuchumi kwa vijana ulioandaliwa na baraza hilo kwa ufadhili wa Taasisi ya Konrad Adenauer Stiftung.

Alisema ni vizuri uchumi ujali utu, mshikamano wa kitaifa na ustawi wa kila mtu.

"Uchumi lazima uwe shirikishi huu mfumo wa uchumi soko jamii tukiupokea Tanzania utabadili nchi kwa haraka kwasababu sisi tunafikiria kama ndugu," alisema.

Alisema viongozi wa dini wanataka kuona maendeleo ya mtu bila kumuacha mtu nyuma. "Tanzania inapaswa kuwa na uchumi wa soko jamii ili kuelekea maendeleo shirikishi na endelevu kiuchumi ambayo yataiwezesha sekta binafsi na mtu mmoja kufanya uwekezaji wenye tija hapa nchini kama ilivyo kwa wawekezaji wa nje," alisema.

Alisema nchi ina rasilimali za kutosha lakini bado kuna tatizo la ajira kwa vijana, uwekezaji mdogo kwa wazawa hivyo suala hilo linapaswa kuondolewa ili wananchi wainuke kiuchumi na kufanya uwekezaji wenye tija.

"Tunao vijana wengi ambao ni nguvu kazi wakipata elimu hiyo kuhusu uchumi wa soko shirikishi utawasaidia kupata elimu hiyo ili kujiajiri wao wenyewe," alisema.

Katibu huyo alisema serikali inapaswa kuendelea kubadili namna ya ufikiri wa vijana wanahitimu vyuo kuwaza kujiajiri wenyewe na badala yake wafundishwe elimu ya uchumi ili wanapomaliza masomo waweze kujiajiri.

Naye Mbunge wa Ubungo, Prof. Kitila Mkumbo, ambaye alimwakilisha Waziri wa Fedha na Mipango alisema wanafunzi wa vyuo wanatakiwa kujitambua na kuwaza kujiajiri na siyo kuajiriwa na taasisi au serikali.

Alisema kuna utafiti ulifanywa na taasisi moja hapa nchini ambayo hakuitaja jina ilionyesha kuwa asilimia 50 pekee ya wanafunzi wanaomaliza vyuo vikuu Afrika Mashariki ndio wenye uwezo wa kuajirika.

Mbunge wa Buchosa, Erick Shigongo aliwataka wanavyuo kutobweteka badala yake shahada walizozipata wazitumie mtaani kutafuta fedha kwa kujiajiri wenyewe.

## Jeshi la Magereza lashauriwa kutoa elimu Sheria ya Parole

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani, Jumanne Sagini, amelitaka Jeshi la Magereza kutoa elimu kwa jamii kuhusu Sheria ya Parole inayowapa fursa wafungwa waliokidhi vigezo vya kwenda kumalizia vifungo vyao nje wasinyanyapaliwe na jamii.

Aidha, amelitaka jeshi hilo kuendelea kuwafuatilia wafungwa waliopata msamaha kupitia sheria hiyo pamoja na wale wa msamaha wa rais ili wasirudie kutenda uhalifu.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini hapa kwenye semina ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na watumishi wa jeshi hilo.

Alisema jamii imekuwa na tatizo la kutokubali kuwapokea wafungwa hao kutokana na uhalifu waliotenda awali jambo ambalo linachangia msongo wa mawazo kwa wafungwa hao.

"Nawapongeza Jeshi la Magereza kwa kuamua kutoa semina hiyo kwa wabunge kwa sababu hawa ni wawakilishi wa wananchi katika majimbo mbalimbali hivyo nao watakwenda kuwa mabalozi wazuri wa kutoa elimu kwa jamii katika maeneo wanayotoka," alisema Sagini.

Awali, Mkuu wa Jeshi la Magereza, Kamishna Jenerali Ramadhan Nyamka alisema lengo la mafunzo hayo ni kutaka kuona jamii inaelewa namna ya utekelezaji wa sheria hiyo na kuomba wabunge kusaidia kutoa elimu kwa wananchi.





# Jeshi la Polisi lapewa siku 7 kumtafuta mwizi wa mahindi

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

JESHI la Polisi wilayani Chunya mkoani Mbeya limepewa wiki moja kuwasaka na kuwasweka ndani watu wanaodaiwa kuiba zaidi ya ekari mbili za mahindi ya mmoja wa wakulima wa Kata ya Lupatingatinga wilayani humo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alitoa agizo hilo wakati wa ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa huo ya kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo wilayani humo pamoja na kusikiliza kero za wananchi.

Homera alisema alipata taarifa kwamba watu hao waliiba mahindi hayo hivi karibuni yakiwa shambani jambo ambalo limemtia hasara mkulima huyo.

Alisema mkulima huyo alitumia gharama kubwa kwenye uzalishaji ikiwamo matumizi ya pembejeo, gharama za kuweka vibarua wa kuhudumia shamba na hivyo kitendo cha kuibiwa ni kumrudisha nyuma.

Alisema ili kukomesha vitendo hivyo, Jeshi la Polisi linatakiwa kufanya msako na kuwakamata wahusika na kuwachukulia hatua kali ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia kama hizo.

"Mtu katumia mbolea na pembejeo zingine, amehudumia mahindi mpaka yamekomaa halafu watu wanakwenda usiku wanavuna, hii ni kazi yenu polisi na nataka ndani ya wiki moja nipate taarifa kwamba mmewasaka na mmewakamata," alisema Homera.

Vilevile alilitaka jeshi hilo kuwasaka vibaka wanaosumbua wananchi katika Mji wa Chunya kwa kuwavizia usiku na kuwapora vitu vyao, huku wengine wakibomoa milango usiku na kuiba vitu.

Baadhi ya wananchi wa Mji wa Chunya, walidai kuwa katika mji huo kuna vibaka ambao huwa wanawasumbua nyakati za usiku wanapotoka kwenye shughuli zao na hivyo kuwafanya wakose amani.

Mmoja wa wananchi hao, Neema Mwakyura, alisema wanapotoka kwenye shughuli zao nyakati za usiku huwa wanakutana na vibaka ambao wananyakua mikoba yao na kutokomea nayo hali ambayo inawatia hofu.

Alisema wakati mwingine wanapokuwa kwenye shughuli zao 'wahuni' wanabomoa milango na kuiba vitu mbalimbali na hivyo akaiomba serikali kuwasaidia kukabiliana na kundi hilo.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka, alisema watahakikisha wanashughulikia tatizo hilo ili wananchi waendelee kufanya shughuli zao kwa amani.

Alisema wananchi wa wilaya hiyo wanajituma kufanya kazi za uzalishaji lakini uwepo wa wahalifu unaweza ukawa kikwazo kwenye uzalishaji huo na hivyo akasisitiza watashughulikia.



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, akikagua ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Sekondari Iwalanje halmashauri ya wilaya hiyo, mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wazazi wapewa angalizo matumizi ya dijitali kwa watoto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAZAZI na walezi wametakiwa kuwaongoza vyema watoto wao kuhusu matumizi sahihi na salama ya kidijitali kwa maelezo kuwa ni moja ya vyanzo vya mmomonyoko wa maadili ndani ya jamii pamoja na ukatili kwa watoto.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Ofisa Maendeleo ya Jamii Kata ya Mbalizi Road jijini Mbeya, Beatha Mtani, wakati akitoa elimu kwa watoto wa Shule ya Msingi Mapinduzi iliyopo katika kata hiyo.

Beatha alisema mtoto anaweza kutazama vitu visivyo na maadili mazuri, vikambadilisha mtazamo na kusababisha maadili yake kubadilika na hivyo akasisitiza kuwa ni jukumu la mzazi au mlezi kuwaongoza watoto wake katika matumizi ya teknolojia.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mapinduzi, Peridah Antony, alisema walimu wanakaa muda mrefu na watoto wawapo shuleni na mara kadhaa huona viashiria vya ukatili.

Alisema ili kukabiliana na tatizo hilo inatakiwa ushirikiano kati ya wazazi na walimu kwenye kukabiliana na matatizo hayo ambayo alisema yanawasababishia watoto maumivu.

Hivyo, aliwasihi wazazi na walezi wanapoitwa na walimu shuleni wasipuuze na kuhisi kusumbuliwa kwa kuwa watoto wao wanaweza wasiwe wawazi kwao na badala yake wakawa wawazi kwa walimu wao na hivyo akaomba ushirikiano.

Mkurugenzi wa taasisi isiyokuwa ya kiserikali ya Sauti ya Mama Afrika (SAMAFO), Tabitha Bugali, alisema wanashirikiana na serikali kutoa elimu katika shule dhidi ya ukatili kwa watoto na kwamba jitihada hizo zimezaa matunda baada ya watoto wengi kuanza kujitambua.

Alisema kwa sasa watoto wengi wako huru kutoa taarifa za viashiria na ukatili huku akisisitiza suala la elimu hiyo kuwa endelevu katika maeneo mbalimbali.

# Wanaoagiza, kufuata bidhaa China wakumbukwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BENKI ya NMB, imeanzisha akaunti maalumu ya sarafu ya kichina (Chinese Yuan) kwa lengo la kuwasaidia wafanyabiashara wa Tanzania wanaofanya malipo na manunuzi mbalimbali nchini China kupata unafuu wa miamala.

Aidha benki hiyo imeanzisha akaunti hiyo kwa lengo la kuwasaidia wafanyabiashara kukabiliana na tatizo la uhaba wa Dola za Kimarekani unaoikabili dunia kwa sasa.

Meneja Mwandamizi wa Fedha na Hazina wa NMB, Joseph Funguguru, aliyasema hayo jijini Mbeya wakati wa chakula cha jioni na mtandao wa wafanyabiashara wakubwa ambao ni wateja wa benki hiyo.

Alisema benki hiyo pia inapokea hati za malipo za sarafu za mataifa mbalimbali ikiwamo ya China, Japan, Afrika Kusini na mataifa mengine ambayo Watanzania wanafanya nayo biashara ili kuwapunguzia adha ya kuhangaika na Dola.

"Lazima tukubali kubadilika kwa sababu hatujui mabadiliko ya kiuchumi duniani, asilimia 80 ya Watanzania kwa sasa wanafanya biashara ya kununua vitu kutoka China na Japan, sasa hakuna ulazima wa hati za malipo kuandikwa kwa Dola, sisi tunapokea na hizo za Chinese Yuan," alisema Funguguru.

Aliwashauri wafanyabiashara kufungua akaunti za sarafu ya kichina kwenye benki hiyo ili waendelee kujiwekea akiba kidogokidogo ambazo zitawasaidia kwenye malipo wanaponunua vitu kutoka China.

Aliwataka Watanzania ambao mpaka sasa hawajafungua akauti Benki ya NMB kufanya hivyo kwa maelezo kuwa ni benki ambayo usalama wa fedha za wateja ni mkubwa na ina matawi na mawakala nchi nzima.

Mkuu wa Kitengo cha Biashara wa NMB, Alex Mgeni, alisema benki hiyo kwa sasa imeanzisha utaratibu wa kuwakopesha wafanyabiashara wadogo maarufu kwa jina la machinga na waendesha bodaboda kwa lengo la kuwainua kiuchumi.

Alisema utoaji wa mikopo hiyo walianzia Zanzibar na kwa sasa wanaendelea kuitoa jijini Dar es Salaam na kwamba wataendelea kupanua mipaka katika mikoa mingine kadri elimu itakavyokuwa inawafikia.

Alisema kundi hilo linatakiwa kupatiwa elimu ya kutosha kabla ya kuanza kukopeshwa ili kuepuka kuanza mivutano ambayo haitakuwa na tija kwenye biashara.

Kaimu Meneja wa NMB Kanda ya Nyanda za Juu, Manyirizu Masanja, alisema benki hiyo imekuwa na utaratibu wa kukutana na wateja wake mara kwa mara kwa lengo la kuwajengea uwezo katika biashara zao ili ziwe endelevu.

Alisema kabla ya kukutana na wafanyabiashara hao wakubwa walikuwa wameshakutana na wafanyabiashara wadogo na wa kati pamoja na wachimbaji na wafanyabiashara wa sekta ya madini katika mkoa wa kimadini wa Chunya.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye hafla hiyo aliipongeza Benki ya NMB kwa ubunifu wa huduma mbalimbali kwa wateja huku akizitaka taasisi zingine za kifedha kuiga mfano.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na benki hiyo kuwasaidia wafanyabiashara kuendelea kuboresha shughuli zao ili kuinua uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.



## SMZ, Urkun zakubaliana ujenzi wa nyumba za wananchi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar na Kampuni ya Urkun Group kutoka Uturuki zimetia saini kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za wananchi eneo la Mangapwani.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, ameeleza hayo jana baada ya kushuhudia zoezi la uwekaji saini ya ujenzi wa nyumba hizo.

Waziri Dk. Khalid alisema serikali itajenga nyumba 370 katika eneo maalum lililotengwa Bumbwini kwa ajili ya kuwafidia wananchi ambao nyumba zao zitabomolewa kupisha ujenzi wa barabara zinaelekea katika eneo la Bandari ya Mangapwani.

Alisema kwamba nyumba hizo zitakuwa za kisasa na zenye ubora ambapo nyumba 240 zitakuwa za vyumba vitatu na nyumba 130 zitakuwa za vyumba vinne.

Waziri Dk. Khalid alisema mfumo huo utawasaidia kwa kiasi kikubwa wananchi ambao hawatalazimika kujenga nyumba badala yake watahama kutoka katika nyumba zao za awali na kuhamia katika nyumba za kisasa.

"Niseme tu serikali imefikia uamuzi huo kwa lengo la kuwasaidia wananchi kwani sote ni mashahidi mara nyingi watu ambao hupewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba zao kwa ajili ya kupisha ujenzi huwa hawafikii malengo walioyakusudia kutokana na changamoto wanazokumbana nazo baada ya kupata fedha zao," alisema.

Aidha, Waziri Dk. Khalid aliwatoa wananchi hofu kwa kusema kwamba, Rais Dk. Hussein Ally Mwinyi tayari ameahidi kwamba hakuna mwananchi atakayedhurumiwa kwa kupisha ujenzi huo kwani serikali italipa na kila mwananchi ataridhika na malipo atakayoyapata.

# ACT-Wazalendo yapinga ripoti ya Tume ya Uchaguzi

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 visiwani Zanzibar ulitawaliwa na uvunjifu wa sheria.

Hayo yalisemwa na Mjumbe wa Kamati Kuu ya chama hicho, Ismail Jussa Ladhu, wakati akichambua Ripoti ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ya mwaka 2020 katika mkutano wa hadhara uliofanyika Paje Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema kwamba chama cha ACT kimeshtushwa na ripoti ya uchaguzi iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa tume hiyo, Jaji Mkuu mstaafu, Hamid Mahmoud kwa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, kueleza uchaguzi huo ulikuwa wa huru na haki.

Jussa alisema kwamba ripoti hiyo haina ukweli wowote, kwamba kulikuwa na uvunjifu wa sheria.

Alisema hata uchaguzi mdogo wa Pandani na Konde kisiwani Pemba ulitawaliwa na vitendo vya uvunjaji wa sheria.

Hata hivyo Jussa alisema ACT-Wazalendo tayari kimejijenga ikiwamo kuteua wajumbe wenye nguvu za hoja watakaoingia kwenye kakosi kazi ya kamati ya maridhiano ambayo itafanya kazi ya kupitia mambo mbalimbali.

Naye Naibu Katibu Uenezi na Habari wa chama hicho, Salum Bimani, alisema kwamba kitendo cha serikali kuvunja masoko matatu kwa pamoja kumechangia kuongeza hali ngumu za maisha kwa wananchi.

Alisema tangu kuvunjwa kwa Soko la Mwanakwerekwe na Jumbi wafanyabiashara wamekuwa wakifanya biashara katika mazingira magumu.

Mshauri wa chama hicho na waziri wa zamani Zanzibar, Mansour Yussuf Himid alisema haikuwa mwafaka kwa Barabara ya Uwanja wa Ndege hadi Mnazimmoja kuvunjwa wakati ilitumia kiwango kikubwa cha fedha kujengwa.

"Hatukatai serikali kujenga barabara kwa sababu watumiaji ni sote lakini kwa nini zinavunjwa barabara nzima zilizotumia kiwango kikubwa cha fedha kwa matengenezo badala ya kujenga barabara mbovu huku ni kutumia vibaya fedha za umma wakati Zanzibar ni nchi masikini," alisema Mansour.

Aidha, alisema ACT-Wazalendo kimeshangazwa na kitendo cha serikali kuteua baadhi ya makatibu wakuu na watendaji katika sekta nyeti kutoka nje ya Zanzibar kinyume na Sheria ya Utumishi ya Zanzibar.

"Tumekua tukipokonywa mamlaka yetu kidogo kidogo sasa tunaletewa watu kutuendesha leo hii benki iliyoasisiwa na Hayati Karume amekabidhiwa mtu kutoka Tanga kuiendesha benki hiyo wanatuambia nini baada ya miaka 60 hakuna Mzanzibar anayeweza kuiendesha benki yetu?" alihoji Mansour.

Aidha alisema Serikali ya Awamu ya Nane pia imeteua baadhi ya makatibu na watendaji katika taasisi nyeti ikiwamo vikosi kutoka nje ya Zanzibar wakati kinyume ni Sheria ya Utumishi wa Umma Zanzibar.

Makamu Mwenyekiti wa Ngome ya Wanawake wa ACT-Wazalendo, Pavu Juma Abdallah, alisema kuna tatizo limejitokeza la watu kupewa mikopo kwa kuzingatia itikadi za kisiasa kitendo ambacho ni kinyuma na Katiba ya Zanzibar.

Alisema fedha za UVIKO-19 ilizotolewa kuwasaidia wajasiriamali zimeshindwa kuwanufaisha wanawake hasa wakereketwa wa vyama vya upinzani jambo ambalo ni kinyume na malengo ya makusudia ya fedha hizo.



Makamu Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo Zanzibar, Othman Masoud Othman, akishiriki ujenzi wa ofisi ya chama hicho, Kijiji cha Shakani Makunduchi Mkoa wa Kusini Unguja. Ikiwa ni mwendelezo wa kukiimarisha chama. **PICHA: RAHMA SYLEIMANI**

## Serikali yatenga bil.12/- kuboresha maslahi ya watumishi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema imetenga Sh. bilioni 12 kwa ajili ya kuimarisha maslahi ya watumishi wa serikali ikiwamo nyongeza za mishahara na posho kwa lengo la kuleta ufanisi wa kazi na kuwatumikia wananchi.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Katiba na Utumishi wa Umma, Haroun Ali Suleiman wakati akizungumza na waandishi wa habari kuelekea maadhimisho ya Siku ya Utumishi.

Alisema serikali imechukua juhudi hizo ikiwamo kuongeza kiwango cha mishahara kwa lengo la kuleta ufanisi na kuwatumikia wananchi kwa uadilifu.

Alisema hakuna sababu kwa watumishi kushindwa kuleta ufanisi katika sehemu za kazi kwa sababu mambo yote ya msingi ikiwamo maslahi na nyongeza katika posho zimezingatiwa.

Alisema imebainika kwa upande wa watumishi wa serikali kumejitokeza vitendo vya utovu wa nidhamu ikiwamo kuchelewa kufika kazini kwa wakati pamoja na dharura nyingi.

"Hizo ni baadhi ya changamoto ambazo tumezibaini kujitokeza katika kipindi cha utumishi wa serikali wakati tukiwa katika maboresho makubwa ya utumishi serikalini," alisema.

Aidha, kwa upande wa watumishi kupoteza uadilifu na uaminifu, alisema ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) zinaonesha wazi kuendelea kuwapo watumishi ambao wanashindwa kuzingatia masharti ya kazi ikiwamo uadilifu.

Alisema katika ripoti hiyo imeonesha katika fedha za miradi ya UVIKO -19 ikiwamo katika ujenzi wa miradi ya shule na hospitali fedha nyingi zimepotea katika manunuzi.

Alisema watendaji wanatakiwa kuacha kuoneana "muhali" na kuwachukulia sheria wafanyakazi wanaokiuka sheria za fedha na matumizi kwa kufanya ubadhirifu.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatarajia kuwasilisha Sheria ya Marekebisho ya Mamlaka ya Kuzuwia Rushwa na Uhujumu Uchumi (ZAECA) kwa ajili ya kuiongezea uwezo kupambana na watumishi na watendaji wabadhirifu wanaotumia fedha za umma vibaya kwa maslahi yao binafsi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**VALENTINE WILLIAM TESHA** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba ya usajili **T 942 BZR**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **MAN/SIM/RB/177432/2023**.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA**
**INAYOKETI DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA RUFAA YA MADAI NA. 304 YA 2019**
**CATHERINE HONORATI............WARUFANI**
**DHIDI YA**

1. **CRDB BANK**
2. **METHOD KAUNGA MORIS.........WAJIBU RUFANI**
3. **HONORATI BIASHARA JOHN LYOMBE**

**KWA:**


1. **METHOD KAUNGA MORIS**
2. **HONORATI BIASHARA JOHN LYOMBE**

**POPOTE WALIPO**

Mnajulishwa kwamba shauri la Rufaa ya Madai tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa katika mahakama kuu Moshi tarehe 3/7/2023 saa tatu kamili asubuhi (3:00)
Mnapaswa kuhudhuria siku na tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hutahudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako anayetambulika kisheria basi rufaa itasikilizwa bila ya uwepo wako.
Imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 14/6/2023

E. G. MRANGU
NAIBU MSAJILI MWANDAMIZI
MAHAKAMA YA RUFANI

## KUPOTEA KWA CHETI



**AUGUSTINO FRANCIS TATUGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0675/018** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia shule ya sekondari Mbugwe mwaka 2006.
Yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**Taarifa ya polisi:MAN/BAB/RB/204847/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JOYCE M ALEXANDA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha **NNE,MWANDETE SECONDARY SCHOOL** chenye Index **No.S 1780-0007** kilichotolewa mwaka 2020 na Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA).
Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:**MWA/NYA/RB/186184/2023**

## TANGAZO KUPOTEA KWA PASSPORT



**MAGAKA SITA NYANGHANI** Anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria( Passport) yenye namba **TAE 404221** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji tarehe **21/5/2021.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awalisiliane na Magaka kwa simu namba **0718026869.**
**Taarifa ya Polisi: SHI/SHI/RB/207884/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**BENJAMINI MADUKANI MWINULA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 520 DDN aina ya TOYOTA- IST,** Chasis **No.NCP600038514.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya polisi **MWA/NYA/RB/206978/202**

**FORM NO. 58**
**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE**
**OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO. 59 OF 2023**

**In Matter of the Estate of the Late**
**MAGAMBO MONGETA NTALLE**

**By 1. ESTHER PAULO MASANJA**
**2. .................................**

All Persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or latter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the **4** day of July, **2023**
Dated at **Morogoro**, this **14** day of **June, 2023**

RESIDENT MAGISTRATE

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

MOB: +255 - 0677020701

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,

WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

## Kesi ya DC aliyestaafishwa kwa lazima yapigwa kalenda

Na Kulwa Mzee

MAHAKAMA Kuu Masjala Kuu imeahirisha shauri la aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Tabora Mjini, Komanya Kitwala, anayepinga uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan kumlazimisha kustaafu bila kumpa sababu hadi Juni 27, mwaka huu kusubiri majibu ya serikali.

Uamuzi huo wa mahakama ulifikiwa jana wakati shauri hilo lilipokuja kwa ajili ya kutajwa kwa mara ya kwanza.

Baada ya kutajwa kwa shauri hilo linalosikilizwa mbele ya Jaji Elizabeth Mkwizu, mahakama ilipanga Juni 27 mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa ili kuangalia kama upande wa serikali utakuwa umewasilisha majibu.

Kitwala amewasilisha maombi dhidi ya Katibu Mkuu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF).

Mwombaji (Kitwala) aliyekuwa mmoja wa wajumbe wa Kamati ya Kuhakiki Mali za Chama Cha Mapinduzi (CCM) iliyoundwa na Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli, aliteuliwa Julai 27, 2018 kuwa Mkuu wa Wilaya ya Tabora Mjini.

Inadaiwa kabla ya uteuzi huo, alikuwa akifanya kazi PSSSF, akiwa Ofisa Sheria. Uteuzi wake ulitenguliwa na Rais Samia Juni 19, 2021 na nafasi yake ilijazwa na Dk. Yahya Ismail Nawanda.

Baada ya uteuzi wake wa U-DC kutenguliwa, alimwandikia barua Katibu Mkuu Utumishi, akiomba amrejeshe katika ajira yake ya awali, PSSF, ambako alikuwa Ofisa Sheria.

Barua hiyo haikujibiwa mapema lakini baadaye alipokea barua ya Katibu Mkuu Kiongozi ya Agosti 15, 2022, iliyomfahamisha kuwa Rais amemstaafisha kwa maslahi ya umma.

Katika shauri hilo la mapitio, Kitwala anaiomba mahakama hiyo iitishe na kisha kutengua na kutupilia mbali uamuzi huo wa Rais kwa kuwa amekwenda nje ya mamlaka yake kisheria dhidi ya kanuni ya haki asili na wa usumbufu kwake.

# Utouh, Zitto waona shida uwajibikaji ripoti za CAG

Na Halfani Chusi

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) mstaafu, Ludovick Utouh, amesema Watanzania wengi hawana uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya uwajibikaji, hali inayosababisha kushindwa kuiwajibisha serikali katika mambo yenye maslahi kwa umma, ikiwamo ubadhirifu wa mali za umma unaoripotiwa na CAG.

Kiongozi huyo ambaye ni Mwasisi wa Taasisi ya Wajibu inayojihusisha na kuchochea uwajibikaji, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam katika mjadala wa pamoja na wadau mbalimbali kuhusu uwajibikaji, bajeti na utaratibu wa utoaji mikopo kwa makundi maalum, maarufu mikopo ya asilimia 10.

Akichangia hoja katika mkutano huo, Utouh aliishauri serikali kuipa uhuru wa kifedha na kiutawala ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani, akiamini itachochea uwajibikaji na kuzuia ubadhirifu wa fedha ambao umekuwa ukiripotiwa kila mara na CAG.

"Tunaishukuru serikali, sisi Wajibu tulipiga kelele kuomba ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani iwe na uwezo wa kifedha na kiutawala, hii ni ofisi iliyoanzishwa mwaka 2012 kutokana na ushauri wa CAG, lakini ikawa haina uwezo wa kifedha.

"Kilichobaki tunakipigia kelele bado mkaguzi huyu hana uhuru wa kikazi, kwa sababu sasa hivi anaripoti kwa bosi wake pale Hazina, ripoti yake haijawa na njia ya kufika kwa mhusika mkuu kwa maana ya Rais na Baraza lake la Mawaziri.

"Likifanyika hilo, Rais na baraza lake watakuwa wanajua ubadhirifu ulipofanyika kabla ya kutoka kwa ripoti ya CAG na kuchukua hatua za kunusuru," alisema Utouh.

Kuhusu mapendekezo ya bajeti ya serikali yaliyowasilishwa bungeni wiki iliyopita, Utouh alisema Watanzania wanapaswa kuiunga mkono kwa kulipa kodi, akisisitiza kuwa bajeti yoyote mahali kokote duniani huwa inazidi uhalisia wa kipato chake.

"Serikali itafanikiwa kuendesha nchi kama sisi wananchi tutatambua umuhimu wa kulipa kodi, na yenyewe inapaswa kutambua fedha inazozisimamia sio za kwao ni za wananchi. Kwa hiyo, inapaswa kutambua kwamba itakuwa na kesi ya kujibu itakapozitumia vibaya," alifafanua.

Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe alisema ili kuchochea uwajibikaji nchini, serikali inapaswa kurejesha mfumo wa demokrasia kama ilivyokuwa awali.

"Kati ya mwaka 2015 hadi 2019, Watanzania milioni nne nchini ambao walikuwa juu ya mstari wa umaskini walidumbukia kwenye dimbwi la umaskini na hiki ndicho kipindi siasa ililala.

"Siasa zikichangamka, watawala wanaelekeza rasilimali fedha kule ambako kuna watu, kwa sababu wanajua tusipofanya hivyo tutahojiwa bungeni au kwenye mikutano," alisema.

Mwandaaji wa mdahalo huo, Mhariri Mtendaji wa The Chanzo, Toni Kirita, alisema lengo lake ni kutaka kujua maoni na uelewa wa wananchi kuhusu uwajibikaji, bajeti, na mikopo kwa makundi maalum.



Diwani mstaafu wa Kata ya Mkuzi, wilayani Muheza mkoani Tanga, Zuberi Semtauwa, akitoa kero yake juzi mbele ya Mkurugenzi mpya wa Halmashauri ya Muheza, Juma Mhina na Mwenyekiti wa Halmashauri Erasto Mhina, katika ukumbi wa halmashauri hiyo, walitoa malalamiko yao kuhusu serikali kushindwa kuwahudumia wazee katika matibabu. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wabunge wataka kuharakishwa miradi ya PPP

Na Jenifer Gilla

KAMATI ya Bunge ya Bajeti imependekeza mambo sita yatakayowezesha kuongeza mauzo na huduma katika sekta nne muhimu zinazochangia upatikanaji wa fedha za kigeni na kukuza uchumi wa nchi ikiwamo utaratibu wa kutumia wabia (PPP), kwenye ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji ili kuchochea skimu za umwagiliaji.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Daniel Sillo aliyasema hayo bungeni jana wakati akisoma taarifa kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2022, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24, tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2022/23 na mapendekezo ya serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Alisema katika kipindi cha hivi karibuni kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa fedha za kigeni nchini, huku zikibainishwa na serikali licha ya kutoeleza sababu za wapi tunapata fedha za kigeni.

"Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba fedha za kigeni nchini kwa kiasi kikubwa zinachangiwa na sekta za kilimo, utalii na madini. Aidha, kuna sekta nyingine ambazo zinachangia lakini siyo kwa kiasi kikubwa kama vile sekta ya viwanda,"alisema.

Alisema mabonde yote ya umwagiliaji yaliyopo chini ya Tume ya Umwagiliaji yanategemea bajeti ya serikali na kupewa kwao msukumo kutasaidia kuwa na kilimo cha uhakika kisichotegemea mvua.

Aidha, kamati hiyo imeishauri serikali kuhakikisha Muswada wa Sheria ya Fedha unawasilishwa bungeni mapema, ili kuipa muda wa kutosha Kamati ya Bajeti kuuchambua, kufanya utafiti na kushirikisha wadau kabla ya kuwasilisha taarifa ya maoni yake bungeni.

Alifafanua kuwa uzoefu wa kamati hiyo unaonyesha muswada huo katika kipindi cha miaka saba haujawahi kusomwa kwa mara ya kwanza na ya pili na kupitishwa ndani ya siku 14 kabla haujapitishwa na Bunge.

Kamati hiyo pia ilishauri kuimarisha miundombinu ya utalii katika hifadhi za taifa, mapori tengefu na malikale ili kuwezesha watalii kufika na kuzuru maeneo hayo, kufanya mapitio ya kodi, ada na tozo ambazo ni kikwazo katika kuongeza mauzo nje ya bidhaa na huduma ili kuchochea ukuaji na utolewaji wa huduma zitakazoliingizia taifa fedha za kigeni.

Pia alisema wanashauri kuchochea mauzo ya dhahabu na makaa ya mawe nje ya nchi na kudhibiti uagizwaji wa bidhaa zisizo za msingi ili kupunguza matumizi ya fedha za kigeni.

Alisema ili kuepuka fedha za mikopo kutumika vilevile alisema serikali imeshauriwa kuhakikisha fedha za mikopo hazitumiki kugharamia matumizi ya kawaida, kuuweka utaratibu wa kukagua shughuli zote za wizara, idara, mamlaka na wakala wa serikali.

HABARI MICHEZO

# SINGIDA FOUNTAIN GATE FC KUJICHIMBIA TUNISIA

Na Shufaa Lyimo

UONGOZI wa timu ya Singida Fountain Gate FC, umesema Bodi ya Wakurugenzi inatarajiwa kukutana mwishoni mwa mwezi huu kwa ajili ya kupanga mikakati kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, itakayoanza kutimua vumbi Agosti mwaka huu.

Akizungumza na mwandishi wetu jana, Msemaji wa Singida Fountain Gate FC, Hussen Masanza, alisema awali waliingia mkataba na Klabu ya US Monastir ya Tunisia kwa ajili ya kuweka kambi ya msimu ujao na kwamba tarehe rasmi itapangwa baada ya bodi hiyo kukutana.

**"Baada ya bodi kukutana ndio tutajua tarehe na mahali ambapo timu yetu itakwenda kuweka kambi kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, hivyo tunaomba mashabiki wetu waondoe hofu," alisema Masanza.**

Alisema baada ya timu hiyo kununuliwa na Fountain Gate hakuna kilichoathirika, hivyo mipango yao ipo palepale na kudai usajili utafanywa kwa kufuata ripoti ya benchi lao la ufundi.

"Usajili utafanywa kwa kufuata ripoti ya benchi letu la ufundi, bodi itafanya maboresho kwenye maeneo ambayo yanahitaji kuongezewa nguvu ili kuhakikisha tunakuwa na timu bora," alisema Masanza.

Alisema kutokana na uwekezaji huo, utasaidia bajeti ambayo itawasaidia kufanya usajili wa wachezaji wenye viwango vya juu.

Aliongeza kuwa timu hiyo itabaki kuwa ile ile isipokuwa itakuwa na malengo makubwa katika kuhakikisha wanafanya vizuri msimu ujao pamoja na mashindano ya kimataifa.

Alisema malengo yao ni kuwa na timu ya kisasa na kuwataka mashabiki wao waendelee kuwa wavumilifu na kuwapa ushirikiano kama kawaida.




Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu, Dk. Kiagho Kilonzo, akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana wakati wa uzinduzi wa filamu ya kisayansi (EONII), inayotarajiwa kuanza kuonyeshwa katika ukumbi wa sinema Mlimani City Ijumaa wiki hii. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Azam FC yaichukua Baobab Queens

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Azam FC imeingia makubaliano ya ushirikiano na wamiliki wa Klabu ya Soka ya Wanawake ya Baobab Queens ya Dodoma ikiwa ni utekelezaji wa agizo la kikanuni la leseni za klabu kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika, CAF.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Hasheem Ibwe, amesema wameingia makubaliano na si kuinunua, kwa sababu kikanuni kuingia makubaliano nayo kupo kwenye kanuni hiyo.

Alisema kutokana na makubaliano hayo, klabu zote mbili zitanufaika, kwa Azam itakuwa imetekeleza utelekezaji wa agizo la CAF, lakini kwa Baobab, itanufaika kwa mambo mbalimbali ikiwamo usafiri, mishahara na masuala mengine ya uendeshaji.

"Hata kama klabu haina timu ya mpira ya wanawake, lakini kanuni itasema inaweza kuingia makubaliano ya ushirikiano na klabu nyingine ya kinadada na ndivyo tulivyofanya, kila klabu itanufaika, na katika makubaliano yetu ni kwamba makao makuu ya klabu hiyo yataendelea kuwa Dodoma," alisema Ibwe.

Klabu hiyo pia ilitoa taarifa rasmi ikionyesha ushirikiano huo kuanzia msimu wa 2024/25.

"Katika kutekeleza agizo la kikanuni la leseni za klabu kutoka Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), Azam FC inayo furaha kuutangazia umma kwamba imeingia makubaliano ya ushirikiano na Klabu ya Soka la Wanawake ya Baobab Queens ya Dodoma.

"Kwa mujibu wa kanuni mpya za CAF, klabu yoyote itakayopata nafasi ya kushiriki mashindano ya Afrika kuanzia msimu wa 2023/24, itapaswa, aidha kuwa na timu ya wanawake au kushirikiana katika uendeshaji na taasisi nyingine yenye timu ya wanawake.

"Kwa makubaliano hayo na Baobab, ni rasmi sasa kwamba klabu hiyo ya Dodoma itakuwa Klabu Dada ya Azam FC kuanzia msimu ujao." Ilieleza taarifa hiyo.

Hivi karibuni, CAF ilitoa maagizo 13 kwa washiriki wote wa klabu zitakazocheza Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho msimu ujao kuwa na timu za wanawake.

Klabu za Simba na Yanga zitakazocheza Ligi ya Mabingwa Afrika zimekuwa na vikosi hivyo, Simba Queens na Yanga Princess kwa muda mrefu, lakini kwa Azam na Singida Big Stars ambazo zitacheza Kombe la Shirikisho mpaka zinapata tiketi hiyo zilikuwa hazina.

Klabu ya Singida Big Stars yenyewe imeuza baadhi ya hisa zake kwa mmiliki wa Klabu ya Fountaina Gate, hivyo kwa sasa inajulikana kama Singida Fountain Gate FC. Klabu hiyo ina timu ya Wanawake Fountain Gate Princess ambayo sasa inaipa uhalali wa kucheza Kombe la Shirikisho msimu ujao.

## TPLB yawashukuru mashabiki Ligi Kuu

Na Abdallah Mataka

MTENDAJI Mkuu wa Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB), Almasi Kasongo, amewashukuru mashabiki na wadau wote wa soka ambao walijitokeza kwa wingi viwanjani kuziunga mkono timu zao tangu msimu wa ligi unaanza mpaka unamalizika, huku akiwataka kuendelea kufanya hivyo msimu ujao ili kuwa sehemu ya kuboresha uchumi wa klabu zao.

Akizungumza na Nipashe jana, Kasongo alisema mashabiki na wadau wa soka wamewaunga mkono kwa kiasi kikubwa tangu msimu wa ligi unaanza mpaka unamalizika, hivyo halitakuwa jambo jema kwa TPLB kama hawatawashukuru.

"Mashabiki wamekuwa wakifika viwanjani hata inapotokea timu zao hazifanyi vizuri, hawaachi kuja, hivyo ni jambo la kuwapongeza sana kwa kuacha shughuli zao na kuja kutazama michezo ya ligi, ni jambo kubwa sana, hiyo inaonyesha ni jinsi gani wanaipa thamani ligi yetu na mchezo wa soka kwa ujumla," alisema Kasongo.

Aidha, alifafanua kuwa moja kati ya vitu vinavyoongeza thamani ya ligi ni kuongezeka kwa watazamaji jambo ambalo mbali na kusaidia klabu kupata mapato lakini huongeza morali kwa wachezaji katika kupata matokeo mazuri.

## Filamu ya EONII kuzinduliwa Dar

Na Shufaa Lyimo

FILAMU ya Kisayansi (EONII) kwa mara ya kwanza inatarajiwa kuzinduliwa Ijumaa wiki hii kwenye Ukumbi wa Sinema wa Mlimani City, Dar es Salaam, imeelezwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Uendeshaji na Uzalishaji wa Vipindi Azam Media, Yahya Mohamed, alisema mbali na Dar es Salaam pia itaonyeshwa mikoa ya Tanga, Arusha, Mwanza, Dodoma pamoja na Visiwani Zanzibar.

Alisema wanatambua mchango mkubwa unaofanywa na serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, katika kuhakikisha sanaa na michezo inazidi kusonga mbele nchini.

"Maandalizi ya filamu hii yamekamilika, tusubiri kuona vitu vitakavyoonyeshwa siku hiyo, vile vile kutakuwa na wageni mbalimbali watakaoshuhudia uzinduzi huo," alisema Mohamed.

Kwa upande wa Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu nchini, Kiagho Kilonzo, alisema filamu hiyo imeandaliwa kwa muda wa miaka minne na kutumia zaidi ya shilingi milioni 400 mpaka kukamilika kwake.

Alisema hiyo itawapa chachu wasanii wengine kukaa na kuandaa vitu ambavyo vitaitangaza nchi yetu kupitia filamu.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### PARTEY SASA KUUZWA

ARSENAL iko tayari kumuuza kiungo wa kati wa Ghana, Thomas Partey, mwenye umri wa miaka 30, msimu huu wa majira ya joto kama sehemu ya marekebisho ya safu yao ya kati.***(Telegraph)***

#### KAI HUYOOO ARSENAL

MCHEZAJI wa Chelsea, Kai Havertz, mwenye umri wa miaka 24, anakaribia kuhamia Arsenal, huku Bayern Munich wakiwa wameachwa kwenye mataa. ***(Sky Sport Germany)***

#### MBAPPE KUBAKI PSG

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe, mwenye umri wa miaka 24, amesema atabaki Paris St-Germain msimu ujao na kuamua mustakabali wake 2024 mkataba wake utakapomalizika. ***(Telefoot, via 90min)***

#### JOSELU SAFI REAL MADRID

REAL Madrid imesema itatangaza kumsajili mshambuliaji wa Hispania, Joselu mwenye umri wa miaka 33, kutoka Espanyol wiki hii na kuondoa uwezekano wa kumnunua Kylian Mbappe msimu huu wa majira ya joto. ***(Sport)***

#### PALHINHA NA WEST HAM

KLABU ya West Ham inaandaa ofa yao ya kwanza kwa Joao Palhinha wa Fulham huku wakimuona kiungo huyo wa kati wa Ureno mwenye umri wa miaka 27, kama mbadala wa Declan Rice. ***(Fabrizio Romano)***

#### SCAMACCA KUTUA ROMA

GIANLUCA Scamacca amekubaliana na AS Roma, huku West Ham ikiwa tayari kumruhusu mshambuliaji huyo wa Italia mwenye umri wa miaka 24, kuondoka kwa mkopo kisha mkataba wa kudumu. ***(Football Insider)***

#### YAKOMAA NA WALKER

BAYERN Munich ipo kwenye mazungumzo ya juu zaidi ya kumsajili beki wa England, Kyle Walker, 33, kutoka Manchester City. ***(Sky Sports)***

#### DISASI AWINDWA UNITED

MLINZI wa Monaco na Ufaransa, Axel Disasi, 25, amebakia kuwa lengo kuu la Manchester United huku beki wa Korea Kusini, Kim Min-jae, 26, akitarajiwa kujiunga na Bayern kutoka Napoli. ***(Fabrizio Romano)***

#### ENRIQUE ATAJWA PSG

KOCHA wa zamani wa Barcelona na Hispania, Luis Enrique, anatarajiwa kuwa kocha mpya wa Paris St-Germain. ***(L'Equipe - in French)***

#### THURAM NA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United iko tayari kuelekeza nguvu zao kwa kiungo wa kati wa Nice ya Ufaransa, Khephren Thuram, 22, baada ya kushindwa kumpata Nicolo Barella wa Inter Milan mwenye miaka 26. ***(Football Insider)***

#### GRIFFITHS KUNG'OLEWA WBA

NEWCASTLE United inaonekana kuwa tayari kutoa ofa ya kushtukiza kwa mlinda mlango wa West Bromwich Albion, Josh Griffiths, 21. ***(Sun)***

## DONDOO OKA MAGAZETI AYA




# HAZARD: BADO SIJAFIKIRIA SUALA LA KUSTAAFU SOKA

**MADRID,** Hispania

EDEN Hazard amefichua kuwa hayuko tayari kustaafu kucheza soka kwa sasa, baada ya kuondoka Real Madrid kama mchezaji huru kwa makubaliano huku akiwa amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake.

**Hazard alifurahia maisha bora katika klabu za Lille na Chelsea, akisaidia kutwaa ubingwa wa ligi na taji la Ufaransa mara mbili mwaka 2011 na kushinda mataji sita makubwa ndani ya miaka saba baadaye.**

Kwa muda mrefu wa miaka ya 2010, winga huyo wa Ubelgiji alizingatiwa kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani.

Cha kusikitisha ni kwamba, uhamisho wake wa mwaka 2019 kwenda Real Madrid wenye thamani ya hadi euro milioni 146 na nyongeza, utakumbukwa kama moja ya uhamisho mbaya zaidi katika historia.

Alikuwa akitoka nyuma ya msimu wake wa ufungaji bora akiwa na Chelsea - mabao 21 katika mashindano yote - na alikuwa muhimu katika mafanikio ya Ligi ya Europa.

Lakini jeraha lilichelewesha mechi yake ya kwanza kule Madrid na mlolongo wa matatizo yaliyoendelea kwa miaka mitatu iliyofuata.

Kwa jumla, Hazard alicheza mechi 76 pekee na mabao saba akiwa na Real Madrid.

Kufikia msimu wa 2022/23, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, alionekana kama angeweza kurudi kwenye ubora wake, lakini badala yake mambo yakazidi kwenda kombo na hivyo kufikia makubaliano ya kusitisha mkataba wake.

Lakini Hazard sasa hataki kuachana na soka baada ya kuwa na muda mbaya kule Los Blancos, kwani anataka kuendelea na kazi yake mahali pengine, badala ya kufuata njia ya kustaafu mapema kama mchezaji mwenzake wa zamani, Gareth Bale.

"Bado ninahisi uwezo wa kuwa mwanasoka wa kulipwa. Nimekuwa nikipumzika kwa miaka miwili au mitatu. Bado nina nguvu kidogo," alisema akiliambia shirika la utangazaji la Ubelgiji, RTBF baada ya kuwa mgeni wa heshima kwenye sare ya bao 1-1 kati ya Ubelgiji na Austria kule Brussels miezi sita baada ya kustaafu kuichezea timu ya taifa.

**Kusema kweli sijui, tumesoma mambo mengi katika siku chache zilizopita na...**

Lakini, kuhusu kuamua ni hatua gani itafuata, Hazard bado hajafanya uamuzi na alipendekeza kuwa uhusiano wa hivi karibuni na Saudi Arabia na klabu isiyojulikana sana ya Ubelgiji RWD Molenbeek bado ni mpana.

"Kusema kweli, sijui bado," alisema. "Baada ya miaka mitatu yenye utata (2019 hadi 2022), ninataka tu kutumia wakati huu na familia yangu, kwenda likizo, kama kila mtu. Tumesoma mambo mengi katika siku chache zilizopita, na upuuzi mwingi."

# NIGERIA YAFUZU AFCON KWA BAO LA JIONI




**MONROVIA,** Sierra Leone

MSHAMBULIAJI Kelechi Iheanacho, alifunga bao la ushindi dakika za lala salama wakati Nigeria ilipoilaza Sierra Leone mabao 3-2 katika mechi ya kufuzu Kombe la Mataifa ya Afrika na kuwa moja ya nchi nne ambazo Jumapili ziliongezwa kwenye orodha ya zilizofuzu kwa mashindano hayo mwakani.

Guinea Bissau pia ilifuzu kutoka Kundi A, huku matumaini ya Sierra Leone yakishindikana, wakati Cape Verde wakitoka Kundi B na Mali kutoka Kundi G.

Wanaungana na wenyeji Ivory Coast, Senegal, Algeria, Burkina Faso, Misri, Equatorial Guinea, Morocco, Afrika Kusini, Tunisia na Zambia katika fainali zitakazofanyika Januari mwakani.

Bao la ushindi la Iheanacho lilileta ahueni kwa Nigeria ambao walikuwa wametangulia kwa mabao 2-0, yaliyofungwa na Victor Osimhen, lakini wakateleza huku Sierra Leone wakisawazisha yote na ubao kusoma 2-2 na kukaribia kufunga la tatu.

Lakini matumaini yao madogo yalimalizwa na mkwaju wa mshambuliaji wa Leicester City, Iheanacho kabla ya kipenga cha mwisho.

Guinea Bissau, ambao walikuwa wamewafunga Sao Tome Jumatano, pia walijihakikishia kumaliza katika nafasi mbili za juu na kufuzu kwa fainali ya nne mfululizo.

Cape Verde, ambayo pia inawavutia sana wachezaji kutoka kwa idadi ya wahamiaji nchini Ureno, iliishinda Burkina Faso mabao 3-1 nyumbani na kujikatia tiketi.

Kiungo wa kati wa zamani wa Manchester United, Bebe alitangulia kufunga kabla ya mabao ya Joao Paulo na Cle kuhakikishia ushindi.

# Silva: Muda si mrefu nitajua wapi nitacheza




**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa kati wa Manchester City, Bernardo Silva, anatumaini kuwa hivi karibuni atakuwa na jibu kuhusu ni wapi atacheza soka lake msimu ujao, huku mchezaji huyo akiwa bado na nia ya kuondoka pale kwenye Uwanja wa Etihad.

Silva alijiunga na City kutoka Monaco kwa pauni milioni 43 msimu wa majira ya joto wa 2017 na ameshinda mataji 12 makubwa katika kipindi chake akiwa Manchester, likiwamo Ligi ya Mabingwa Ulaya mapema mwezi huu.

Amecheza zaidi ya mechi 300 akiwa na City na kwa kawaida amekuwa kwenye kikosi cha kwanza muda wote.

Siku mbili tu baada ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Silva aliitaarifu klabu hiyo kuwa anataka kuondoka.

"Nitakuwa mkweli sana, sijui. Tutaona siku chache zijazo. Hata kama ningejua, haingekuwa nafasi ya kulizungumzia katika majukumu ya mechi za kimataifa," alisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, akiiambia Eleven Sports alipoulizwa kuhusu mustakabali wake kabla ya ushindi wa Ureno wa kufuzu kwa Euro 2024 dhidi ya Bosnia & Herzegovina.

Barcelona na Paris Saint-Germain zimekuwa klabu zinazohusishwa mara kwa mara na Silva katika miezi ya hivi karibuni.

90minutes ilifichulia mwanzoni mwa Mei kwamba, City ambao wamekuwa tayari kuwauza wachezaji kama Raheem Sterling, Gabriel Jesus na Oleksandr Zinchenko hivi karibuni, hawatazuia uhamisho wa majira ya joto iwapo klabu itakuwa tayari kukidhi thamani ya wachezaji wake akiwamo Silva.

# Southgate asifia ufungaji mabao wa Rashford

**LONDON,** Engand

KOCHA wa England, Gareth Southgate, amepongeza "maendeleo makubwa" katika ufungaji wa mabao wa Marcus Rashford na kusisitiza kuwa fowadi huyo wa Manchester United "anapenda" kuichezea nchi yake.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, amefunga mabao nane katika mechi 17 zilizopita za kimataifa, yakiwamo matatu kwenye Kombe la Dunia la 2022.

Akiwa amefunga mabao saba pekee katika mechi zake 35 za kwanza, rekodi iliyoboreshwa ya hivi karibuni ya Rashford imeakisi silika yake mpya ya muuaji katika ngazi ya klabu.

Alimaliza msimu akiwa na mabao 30 katika mechi 56 alizochezea United huku Southgate akisifu matokeo yake mazuri.

"Jambo lililo wazi ni mabao," alijibu alipoulizwa ni nini Rashford ameleta kwenye mchezo wake.

"Nadhani wakati amepata nafasi msimu huu unatarajia atafunga kama msimu unaendelea.

"Nadhani, katika kufanya kazi na Erik (ten Hag), imebidi afanye kazi tofauti kidogo bila mpira. Kumekuwa na jukumu zaidi juu ya hilo kama timu. Naweza kusema hesabu ya mabao ni maendeleo makubwa kwake na kitu ambacho atakifurahia.

"Kwa sasa bado nadhani yeye ni bora kutoka kushoto kuliko kama namba tisa, lakini bila shaka amepiga hatua akicheza namba tisa mwaka huu na alikuwa na mchango mkubwa."

Rashford aliingia kipindi cha pili kwenye ushindi wa Ijumaa wa mabao 4-0 kule Malta huku England ikidumisha mwanzo wao wa asilimia 100 wa kampeni ya kufuzu kwa Euro 2024.



## TRA yaja na bonanza kwa wafanyabiashara

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Kikodi Ilala, imeandaa bonanza la michezo kati yao na Wafanyabiashara wa Kariakoo, litakalofanyika katika viwanja vya Michezo vya Jakaya Kikwete, Kidongo Chekundu Julai Mosi, mwaka huu.

Meneja wa Kodi Kariakoo, Mkoa wa Kikodi Ilala, Alex Katundu, amesema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kusogeza huduma karibu na wafanyabiashara.

Alisema bonanza hilo litahusisha michezo mbalimbali itakayowafanya kuendelea kushirikiana na kufanya kazi kwa ukaribu zaidi.

"TRA Mkoa wa Kikodi Ilala, tumeandaa bonanza kubwa litakaloshirikisha wadau wetu hususan wafanyabiashara, tunaamini michezo ni furaha, afya, amani na inatuunganisha na kutengeneza daraja la kutuunganisha katika kupigania maslahi mapana ya nchi," alisema Katundu.

Alisema bonanza kama hilo limeshawahi kufanyika siku za nyuma hivyo ni mwendelezo wa kuendelea kushirikiana katika kuhakikisha wanaoboresha huduma na wateja wao.

Sambamba na hilo alisema wameendelea kusogeza huduma karibu na wananchi kwa kutenga maeneo matatu katika mitaa ya Kariakoo ili kuwahudumia, kutoa kontroo namba na kupokea maoni ya changamoto za wafanyabiashara hao.

## Yanga na hatima ya Kaze, Bangala

INATOKA UKURASA 24

tukisubiri kumpata mwalimu mpya, lakini tunaongea na mchezaji mwenyewe, halafu hatima yake itatolewa. Apata ofa, klabu ikasikiliza kama inakuwa na maslahi ya pande zote basi itamruhusu, lakini mpaka tunavyozungumza Bangala bado ni mchezaji halali wa Yanga," alisema.

Kuhusu kuachana na Tuisila Kisinda, Kamwe alisema amemaliza mkataba wake wa mwaka mmoja kutoka klabu ya RS Berkane na sasa anarejea huko.



Bangala

# KOCHA STARS ATAKA NIGER IBURUZWE CAF MAPEMA

**Na Saada Akida**

HUKU Timu ya Taifa ya Niger ikianika mkakati wake wa kwenda kupanga matokeo kwa kuibeba Uganda kwenye mechi ya mwisho, Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Adel Amrouche, amelalamikia mpango huo mchafu kwa maendeleo ya soka la Afrika, lakini akisema ataendelea kujenga timu bora kwa kuwaita wachezaji vijana kwa ajili ya faida ya hapo baadaye.

Taifa Stars juzi ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Niger kwenye mchezo wa kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) mwakani nchini Ivory Coast, uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Akizungumza na Nipashe jana, Amrouche alisema wamefanikiwa kupata matokeo mazuri ambayo yanawapa matumaini ya kufuzu kucheza michuano hiyo licha ya kuwapo kwa mapungufu ya kutotumia nafasi wanazotengeneza.**

"Ninaimani kubwa na wachezaji hawa vijana ambao watakuwa msaada mkubwa kwa hapo baadaye, nitaendelea kuwatumia ili kutengeneza uwiano mzuri wa timu tishio na kufanya vizuri katika michuano ijayo.

"Wachezaji wengi kwa sasa ligi zimeisha, miongoni mwao wamechoka wanahitaji kupumzika na wengine walikuwa tayari wapo kwenye mapumziko yao baada ya msimu ndio maana leo hatujacheza vizuri, nimefurahishwa sana na kijana Morice Abraham hii ni nafasi kwangu kuwapa nafasi wachezaji vijana kwa ajili ya Stars ya kesho," alisema kocha huyo.

Amrouche alisema baada ya mchezo huo juzi, kocha msaidizi wa Niger aliweka wazi kuwa wataenda kuwaachia Uganda wawafunge kwa sababu hawajafurahishwa na matokeo yetu ya kushinda.

"Wamesema wanaenda kuwaachia Uganda mchezo wa mwisho ili wao ndio wafuzu AFCON, nafikiria hii si sawa na sio 'Fair Play' (mchezo wa kiuungwana), tunabidi tuliwasilishe hili mapema kwa mamlaka husika," alisema Amrouche.

Kwa matokeo hayo, Stars sasa inashika nafasi ya pili ikiwa na pointi saba nyuma ya vinara Algeria wenye alama 15 huku Uganda ikiwa nafasi ya tatu na pointi zao nne kwenye Kundi hilo la F.

Niger inayoburuza mkia ikiwa na pointi mbili hadi sasa, imepoteza nafasi ya kufuzu kwa fainali hizo hata kama itashinda mchezo wake wa mwisho nyumbani dhidi ya Uganda.



Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Saidi Yakubu (wa pili kushoto), akishiriki mazoezi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Yoga Duniani inayoadhimishwa Juni 18, kila mwaka. Maadhimisho hayo kwa Tanzania yalifanyika katika viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na watu mbalimbali akiwamo Balozi wa India nchini, Binaya Srikanta Pradhan (kulia) na Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa nchini, Zlatan Miliši. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Miquissone aitoa jasho Simba*

INATOKA UKURASA 24

Wakati huo huo mabosi hao imeelezwa tayari wamefanikiwa kuinasa saini ya winga wa kulia wa Kimataifa wa Niger, Victorien Adebayor, ikiwa ni muda mchache kabla ya kuivaa Taifa Stars juzi, Jumapili.

Mabosi wa timu hiyo wamekuwa wakipambana kuhakikisha wanaijenga upya timu yao kutokana na kufanya vibaya msimu uliopita kwa kushindwa kushinda kombe lolote la kimashindano ambapo kwenye Ligi Kuu Bara wamemaliza katika nafasi ya pili nyuma ya mabingwa, Yanga wakati kwenye Kombe la FA wakiishia nusu fainali huku Ligi ya Mabingwa mwisho wao ukiwa robo fainali.

Taarifa za uhakika kutoka chanzo chetu ndani ya timu hiyo, zimeeleza kuwa Simba wamekubaliana kila kitu na winga huyo juu ya kujiunga na timu hiyo katika msimu ujao wa Ligi Kuu Bara na michuano ya kimataifa kwa mkataba wa miaka miwili na kilichobakí ni kwenda kumalizana na klabu yake, RS Berkane.

Michezo
Jumanne Juni 20, 2023
Nipashe



Kocha Stars ataka Niger iburuzwe CAF

UKURASA 23

# Miquissone aitoa jasho Simba SC

## Dili laiva, tatizo ni mshahara wake, waiangukia Al Ahly wasaidiane...

**Na Saada Akida**

DILI la kiungo mshambuliaji wa Al Ahly, Luis Miquissone, kurejea klabu yake ya zamani, Simba kuelekea msimu mpya wa 2023/24, ni kama limefikia asilimia 80, lakini shida ni maslahi binafsi ya winga huyo hatari, imeelezwa.

**Wakati wowote nyota huyo anaweza kutua ndani ya kikosi cha Simba kwa ajili ya kuwa sehemu ya kukiimarisha kuelekea michuano ya Super League, Ligi ya Mabingwa Afrika na Ligi Kuu Tanzania Bara.**

Miquissone hana nafasi ndani ya kikosi cha Al Ahly na tayari miamba hiyo imemweka sokoni nyota huyo raia wa Msumbiji baada ya mkataba wake wa mkopo wa kuichezea Klabu ya Abha inayoshiriki Ligi Kuu nchini Saudi Arabia kufikia tamati na kurejea kwao kwa sasa akifanya mazoezi binafsi.

Taarifa za uhakika zilizolifikia Nipashe jana kutoka chanzo makini ndani ya klabu hiyo, zimeeleza kuwa uongozi wa Simba umelipitisha jina la Miquissone kuwa usajili wao mkubwa msimu ujao kupitia dirisha kubwa ambalo litafunguliwa hivi karibuni.

Chanzo hicho kilisema kuwa uongozi wa Simba uko katika mazungumzo na Al Ahly kwa ajili ya makubaliano maalum ili kuweza kupata huduma ya nyota huyo kutokana na masharti ya klabu hiyo kwa Miquissone.

"Miquissone kwa sasa hana nafasi tena katika kikosi cha Al Ahly ambao wanahitaji kumuuza lakini kutokana na dau kubwa waliloweka la kumnunua mchezaji huyo pia naye anataka mshahara wake ule ule unaofikia milioni 80 kwa mwezi, ambazo kwa hapa Tanzania ni ngumu kumlipa.

"Kwa kuwa tunahitaji huduma ya mchezaji huyo tunafanya mazungumzo na Al Ahly ikiwezekana wao wawe wanamlipa asilimia 75 (milioni 60) katika mshahara wake na sisi Simba tutoe asilimia 25 (milioni 20)," kilisema chanzo hicho makini.

Kilisema kwa sasa Miquissone hayupo ndani ya Al Ahly baada ya klabu hiyo kumtoa kwenye mipango yao na kusema wapo tayari kumuuza.

"Simba wana mpango wa kumrudisha Miquissone ndani ya timu hiyo na kuwa usajili wao mkubwa wakiamini wanaweza kumpata kutokana mahusiano mazuri baina yao na Al Ahly, kwa sasa wanatakiwa kukubaliana maombi hayo ili kuweza kupata huduma ya nyota huyo," kiliongeza.

INAENDELEA UKURASA 23



# Yanga na hatima ya Kaze, Bangala

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema hatima ya aliyekuwa kocha wake msaidizi Cedric Kaze, itafahamika mara baada ya kupatikana kwa kocha mkuu, huku pia ikiweka wazi kila kitu kuhusu Yannick na Tuisila Kisinda ndani ya kikosi hicho.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, amesema kwa sasa wapo kwenye mchakato wa kumpata Kocha Mkuu na atakapokabidhiwa majukumu ndiye atakayeamua kuendelea kufanya kazi na benchi lililopo akiwamo Kaze, au kuja na watu wake.

Kutokana na hali hiyo, hatima ya kocha huyo raia wa Burundi kubaki Yanga au kuondoka, itategemea maamuzi ya kocha atakayekuja.

"Sasa hivi mazungumzo yaliyopo ni kumpata kocha mkuu, tukishampaka ndiyo tunampa fursa mwalimu anayekuja kuchagua wasaidizi wake, akitoa ruhusa tutaendelea na mazungumzo, yeye ndiye atakayetuambia watu gani anaotaka kufanya nao kazi kwenye benchi lake la ufundi.

"Akisema anawahitaji sawa, lakini anaweza kusema anakuja na benchi lake la ufundi, ndiyo dunia ya mpira wa sasa ilipofikia na sisi Yanga ni weledi," alisema Kamwe.

Akizungumzia juu ya taarifa za mchezaji wao Bangala kutaka kuondoka, alisema kwa sasa ni mchezaji wa Yanga aliyebakisha mwaka mmoja, lakini kama akipata ofa nono, yenye maslahi kwa pande zote mbili klabu haiwezi kumzuia.

"Mpaka sasa ana mkataba wa mwaka mmoja, na mwaka wake uliobakia tunapitia ripoti ya benchi la ufundi,

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >